# KUCHUNGUZA VIAMBISHI NJEO NA HALI KATIKA LAHAJA YA KITUMBATU

**BISHARA NASSOR MOH'D**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKIDHI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## ITHIBATI

Aliyeweka saini hapo chini anathibitisha kuwa ameisoma kazi hii ambayo ina mada, "***Kuchunguza Viambishi Njeo na Hali katika Lahaja ya Kitumbatu,"*** na anapendekeza ikubaliwe kwa kuwa imekidhi masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

**…………………………………….**

**Hanna J. Simpassa**

**(Msimamizi)**

**Tarehe……….……………………..**

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga, kunakili kwa namna yoyote na kwalengo lolote tasnifu hii bila ya idhini ya mmiliki au Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi **Bishara Nassor Moh'd** nathibitisha kuwa kazi hii ni yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa chuo kikuu chochote kile kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine.

**……………………..……………**

**Saini**

**Tarehe……………………………..**

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa; Bibi Mchanga Nassor Suleiman na baba yangu Bwana Nassor Mohammed Abdallah kwa kunilea katika malezi yanayoendana na maadili ya Wazanzibari. Aidha naitabaruku kwa mume wangu mpenzi Bwana Rajabu Khamisi Hamad kwa kuniliwaza, kunivumilia na kunipa moyo katika wakati mgumu wa masomo yangu. Pia naitabaruku kazi hii kwa mtoto wangu kipenzi Nassor Idrissa Saleh kwa kuweza kuvumilia katika kipindi chote cha masomo yangu. Naitabaruku tena kazi yangu hii kwa muanzilishi na mfunguzi wangu wa fursa ya kujisomea elimu ya juu baba wa mtoto wangu marehemu Idrissa Swaleh Omar. Mwenyezi Mungu amsamehe, amrehemu na ampe makazi katika pepo yake. **(AMIN)**

## SHUKRANI

Kabla ya yote natoa shukrani zangu za dhati na za pekee kwa Mwenyezi Mungu aliyeumba mbigu na ardhi aliyenipa subra, nguvu, uwezo na pumzi ya kuweza kutafiti, kuandika na kukamilisha kazi hii. Ni kweli kuwa bila yeye nisingeweza kufanya lolote. Aidha, nawashukuru waalimu na wataalamu mbali mbali waliosababisha kukamilika kazi hii akiwemo mwalim Bakari Kombo Bakari. Pia, namshukuru kwa dhati msimamizi wa kazi hii mwalim wangu Dkt. Hanna Simpassa kwa kuweza kuninisukuma kila ninaposimama. Michango yao ya hali na mali nakiri kwamba ilinisaidia.

Nitakuwa mwizi wa shukuri kwa kuacha kuwashukuru wazazi wangu Bi Mchanga Nassor Suleiman, baba mzazi Bwana Nassor Mohammed Abdalluh na baba yangu mlezi mzee Said Rashid Aliy. Pia sina budi kumshukuru nyongo mkalia ini mume wangu kipenzi Bwana Rajabu Khamis Hamad kwa kunivumilia katika kipindi kigumu alichokumbana nacho wakati wa masomo yangu. Pia sitoacha kumsahau mwanangu Nassor Idrisa kwa kuwa mvumilivu kutokana na kuwa mbali na mama yake kwa kipindi kirefu.

Kiujumla, nawashukuru wote waliotoa mchango wao katika kazi hii, niliowataja na nisiowataja wakiwemo maprofesa, madaktari, waalimu, watoataarifa, majirani, ndugu na jamaa, nawaomba radhi kwa kutowataja hapa ila kiukweli naomba waamini kwamba michango yao imekuwa msaada mkubwa kwangu. Nimeipokea na kuifanyia kazi ilipobidi. Nawaambia ahsanteni. Mwenyezi Mungu awajaze imani na awape wepesi katika maisha yenu. (**AMIN)**

## IKSIRI

Tasnifu hii ilihusu Uchunguzi wa Viambis injeo na Hali katika Lahaja ya Kitumbatu. Utafiti huu ulifanyika katika shehiya mbili za jimbo la Kiwani, shehia ya Mwambe na shehia ya Jombwe, katika vijiji vya Tasni, Bwegeza, Chanjani na Mwambe. Jumla ya watafitiwa 50 ya vijana na wazee walioishi Utumbatuni kwa muda mrefu walishiriki katika utafiti.Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi mawili; lengo la kwanza ni kubainisha viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu, na lengo la pili ni kuchanganua athari za kimofofonolojia zinazojitokeza katika vitenzi vya Kitumbatu wakati wa kudhihirisha viambishi njeo na hali. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya Dodoso, usaili na uchunguzi makini kisha kachambiliwa kwa kutumia mkabala usio wa kiidadi (maelezo) kwa kuongozwa na nadharia ya mofofonolojia ya Trubezkoy ya (1929). Matokeo ya utafiti yameonyesha kwamba njeo za nyakati na hali mbalimbali zilizojitokeza na michakato ya kimofofonolojia imedhihirishwa na mabadiliko ya miundo, kutoka muundo ndani kwenda miundo nje. Mabadiliko hayo yamedhihiri kupitia kanuni mbalimbali za kimofofonolojia kama vile udondoshaji, uyeyushaji na tangamano lairabu. Mtafiti amependekeza kuwa tafiti zijazo zijfanye utafiti zaidi juu ya uchambuzi wa kimofosintaksia za lahaja zifanyike, ili kubaini jinsi viambishi vya njeo vinavyoathiri vitenzi vya lahaja husika. Pili, mtafiti amependekeza kwamba tafiti nyingine za Kimofofonolojia zifanywe kwenye lugha za Kibantu ili kubaini kwa kiasi gani vitenzi vya Kibantu huathirika kutokana na michakato ya kimofofonolojia.

# YALIYOMO

ITHIBATI ..... i

HAKIMILIKI ..... ii

TAMKO ..... iii

TABARUKU ..... iv

SHUKRANI ..... v

IKSIRI ..... vi

YALIYOMO ..... vii

ORODHA YA MAJEDWALI ..... xi

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA ..... 1**

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Usuli wa Utafiti ..... 2

1.3 Tatizo la Utafiti ..... 3

1.4 Malengo ya Utafiti ..... 4

1.4.1 Lengo Kuu ..... 4

1.4.2 Malengo Mahsusi ..... 4

1.4.3 Maswali ya Utafiti ..... 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti ..... 4

1 .6 Mipaka ya Utafiti ..... 5

1.7 Changamoto za Utafiti ..... 5

1.8 Mpanglio wa Utafiti ..... 6

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ........ 7**

2.1 Utangulizi ........ 7

2.2 Fasili ya Lahaja ........ 7

2.3 Lahaja ya Kitumbatu ........ 8

2.4 Dhana ya Mofolojia ........ 8

2.5 Dhana ya Mofofonolojia ........ 8

2.6 Dhana ya Kiambishi ........ 9

2.7 Dhana ya Njeo ........ 10

2.8 Dhana ya Kiambishi Njeo ........ 10

2.9 Viambishi Njeo vya Kiswahili ........ 10

2.10 Dhana ya Hali ........ 11

2.11 Kazi Tangulizi ........ 12

2.12 Kiunzi cha Nadharia ........ 17

2.13 Muhtasari wa Sura ........ 18

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........ 19**

3.1 Utangulizi ........ 19

3.2 Mkabala wa Kiutafiti ........ 19

3.3 Eneo la Utafiti ........ 19

3.4 Sampuli na Usampulishaji ........ 20

3.5 Mbinu za Kukusanya Data ........ 21

3.51 Dodoso ........ 22

3.5.2 Uchunguzi Makini ........ 24

3.5. 3 Mbinu ya Usaili ........ 24
3.6 Mbinu za Kuchambua Data ........ 26
3.6.1 Maana ya Data ........ 26
3.6.2 Uchambuzi wa Data ........ 26
3.7 Misingi ya Maadili ........ 27
3.8 Muhtasari wa Sura ........ 27

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UFAFANUZI NA UCHANGANUZI WA DATA ........ 28**

4.1 Utangulizi ........ 28
4.2 Viambishi Njeo katika Lahaja ya Kitumbatu ........ 28
4.2.1 Kiambishi Njeo Kinachowakilisha Wakati Uliopita katika Lahaja ya Kitumbatu katika Kitenzi cha Kawaida ........ 29
4.2.2 Kiambishi kinachowakilisha Njeo ya Wakati Ulipita katik Kitezi kilichoanza na Iarbu /i/, /e/, /o/ na irabu /u/ katika Mzizi ........ 31
4.2.3 Kiambishi kinachowakilkisha Njeo ya Wakati uliopo katika Lahaja ya Kitumbatu ........ 35
4.2.4 Kiambishi Njeo kinachowakilisha Wakati Unaokuja katika Lahaja ya Kitumbatu ........ 37
4.2.5 Kiambishi Kinachowakilisha Haliya Ushuruti katika Lahaja ya Kitumbatu ........ 39
4.2.6 Kiambishi kinachowakilisha Hali ya Mazoea ........ 40
4.2.7 Kimbishi Kinachowakilisha Hali ya Kuendelea kwa Tendo Katika Lahaja ya Kitumbatu ........ 41

4.3 Uchambuzi wa Kimofosinaksia .................................................................. 42

4.3.1 Athari za Kimofofonolijia zinazojitokeza katika Lahaja ya Kitumbatu ........ 42

4.3.2 Athari za Kimofofonolojia zinazojitokeza katika Lahaja ya Kitumbatu Katika Njeo ya Wakati uliopita kwa Kitenzi cha Kawaida Uyakinishi ......... 43

4.3.3 Athari za Kimofofonolojia Zinazojitokeza katika Hali ya Ukanushi ............ 44

4.4 Athari za Kimofofonolojia Zinazojitokeza Kwenye Vitenzi vya Lahaja ya Kitumbatu Katika Njeo ya Wakati Uliopita Katika Hali ya Uyakinishi na Hali ya Ukanushi .................................................................. 46

4.5 Athari za Kimofofonolojia zinazojitokeza katika Wakati Ujao..................... 47

4.6 Athari za kimofofonolojia zinazojitokeza katika Njeo inayowakilisha Hali Timilifu .................................................................................. 48

4.7 Athari za Kimofofonolojia zinazojitokeza katika Hali ya Mazoea................ 48

4.8 Ufaafu wa Kinadharia ...................................................................... 49

4.9 Hitimisho.................................................................................. 50

**SURA YA TANO ......................................................................................... 51**

5.1 Utangulizi.................................................................................. 51

5.2 Muhtasari wa Utafiti ...................................................................... 51

5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ................................................................ 51

5.4 Hitimisho.................................................................................. 53

5.5 Mapendekezo .............................................................................. 53

**MAREJELEO ............................................................................................ 54**

**VIAMBATISHO ......................................................................................... 57**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na.2.1 Tofauti ya lahaja ya Kusini Pemba na Kaskazini Pemba ............ 8

Jedwali Na.2.2 Vambishi Njeo vya Kiswahili .................................................. 11

Jedwali Na.2.3 Tofauti ya Viambishio Njeo na Hali baina ya Kipemba na Kiswahili Sanifu (KS) ............................................................ 15

Jedwali Na. 2:4 Njeo Za Nyakati Mbali Mbali Katika Kiswahili Sanifu............. 16

Jedwali Na.3.1 Watoa Taariafa ........................................................................ 21

Jedwali na.4:1 Viambishi Njeo vya Hali ya Uyakinishi na Hali ya Ukanushi katikaLahaja ya Kitumbatu....................................................... 29

Jedwali na. 4:2 Jinsi Kiambishi cha Njeo Wakati uliopita Kinavyofanya Kazi .. 30

Jedwali na. 4.3 Viambishi Njeo vinavyowakilisha Wakati uliopita katika Vitezi vilivyoanza na Irabu -/i-/ katika Mzizi ........................... 31

Jedweli na. 4.4 Viambishi Njeo Vinavyowakilisha Wakati Uliopita katika Vitenzi vilivyoanza na Irabu /-e-/ katika Mzizi.......................... 32

Jedwali Na: 4.5 Viambishi Njeo vinavyowiakilisha Wakati uliopita katika Vitenzi vilivyoanza Irabu /-o-/ katika mzizi............................. 32

Jedwali Na. 4.6 Viambishi Njeo vinavyowakilisha Wakati uliopita vilivyoanza na Irabu /-u-/ katika Mzizi........................................................ 33

Jedweli Na. 4.7 Viambishi njeo vinavyowakilisha Wakati uliopita Vilivyoanza na Irabu /-a -/ katika Mzizi ........................................................ 33

Jedwali na. 4.8 kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati uliopo katika Lahaja ya Kitumbatu ................................................................ 36

Jedwali Na. 4.9 Kiambishi kinachowaklisha Njeo ya Wakati ujao...................... 37

Jedwali Na. 4.10: Kiambishi kinachowaklisha Njeo ya Wakati ujao Ukanushi (z+-----------Ti) ........................................................................ 38

Jedwali Na 4.11 (a): Kiambishi –nge- katika Hali ya Ushuruti ................................ 39

Jedwali Na. 4.11(b) Kiambishi cha Sharti –ka- na Ukanushi wake kinavyodhihiri katika Lahaja ya Kitumbatu....................................................... 40

Jedwali Na 4.12 Kiambishi kinachowakilisha Hali ya Mazoea ........................... 41

Jedwali na 4.13 Kiambishi Hali "ka" kinachowakilisha Kuendelea kwa Tendo 42

Jedwali na.4.14 Vitenzi vya Kitumbatu Vinavyoonesha Wakati Uliopita Yakinishi katika Nafsi ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu ............... 43

Jedwali na 4.15 Vitenzi vya Kitumbatu vinavyoonesha Wakati uliopita Kanushi.......................................................................... 44

Jedwali na. 4.16 Vitenzi vya Kitumbatu Vinavoonesha Wakati Uliopo Katika Hali ya Uyakinishi na Ukanushi ................................................ 46

Jedwali na 4.17 Vitenzi vya Kitumbatu vinavyoonesha Njeo inayowakilisha Wakati Ujao................................................................... 47

Jedwali na. 4.18 Vitenzi vya Kitumbatu vinavyowakilisha Hali Timilifu ............ 48

Jedwali na: 4.19 Vitenzi vya Kitumbatu vinavyoonesha Njeo inayowakilisha hali ya mazoea ........................................................................ 49

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulikuwa na shabaha ya kuchunguza viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu kwa kujikita zaidi kwenye uchambuzi wa kimofonolojia. Mtafiti wa kazi hii ameamua kuteuwa mada hii kwa sababu ameona kwamba umbo la msingi la kitenzi cha Kitumbatu huathirika sana baada ya kuingizwa kiambishi njeo, hivyo akataka kujua ni kipi hujitokeza na kuleta athari hii kubwa. Kwa msingi huu uchambuzi wa kimofolojia ameuona kuwa ni wa msingi ili kubaini mabadilko hayo.

Kisiwa cha Tumbatu kipo kaskazini magharibi ya kisiwa cha Unguja. Kisiwa hiki nisehemu ya Wilaya ya ya Kaskazini "A". Kisiwa cha Tumbatu kimo ndaniya mkoa wa kaskazini Unguja na ni kisiwa cha tatu kwa ukubwa Zanzibar baada ya kisiwa cha Fundo kilichoko Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba na Kisiwa Panza kilichoko Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba. Tumbatu kina maeneo miwili makubwa. Eneo la kwanza ni Jongowe ambao liko kusini mwa kisiwa hicho na Kichangani ambalo liko kaskazini ya kisiwa hicho. Kwa mujibu wa Ali (2016) kisiwa cha Tumbutu kiko umbali wa kilomita 46.7 kutoka mjini Unguja na kiko masafa ya kilomita tatu kutoka ghuba ya Mkokotoni. Kwa upande wa kaskazini mashariki kisiwa hiki kimepakana na maeneo ya Nungwi. Wakaazi wa kiswa cha Tumbatu wanazungumza Kiswahili cha Tumbatu (lahaja ya Kitumbatu).

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Tafiti nyingi kuhusiana na Lugha ya Kiswahili na lahaja zake zimefanywa. Miongoni mwa tafiti ambazo mtafiti wa kazi hii amekutana nazo ni pamoja na ile ya Whitely (1958) aliyechunguza vipengele vya kiisimu katika lahaja ya Kimtang'ata. Lambert (1957, 1958) aliyechunguza vipengele vya kisarufi katika lahaja za Kenya, zikiwemo Kivumba, Chi-jomvu, Kingare na Chichifundi. Chum na Lambert (1963:87-89) waliochunguza sarufi iliyotumika katika vita vya Uhud Saudia Rabia. Khamis (1984) aliyetafiti kuhusu ulinganishi kati ya Kipemba cha mjini na kile cha vijijini. Said (2011) aliyechunguza viangama katika lahaja ya Kipemba. Makame (2015) na Masoud (2016) na wao pia wameangalia kuhusu viangama. Makame aliangalia viangama kwenye lugha ya Mazungumzo Mjini Unguja, ilhali Masoud aliangalia viangama kwenye lahaja ya Kitumbatu. Kuhusu tafiti zilizofanywa kuhusiana na viambishi njeo katika Kiswahili na lahaja zake mtafiti amebaini kwamba kazi kadhaa kwenye eneo hili zimefanywa. Miongoni mwa kazi hizo ni ile ya Maganga (1995) ambae alichunguza Mofofonolojia ya Lahaja za visiwani (Kswahili, Kimakunduchi, Kipemba na Kitumbatu). Pamoja na mambo mengine katika uchambuzi wake Maganga (keshatajwa) alidokeza mdhihiriko wa viambishi njeo juu ya lahaja hizo.

Mwingine aliyeangazia eneo hili ni Hamad (2011), aliyeonesha mdhihiriko wa viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu, huku akijikita zaidi kwenye ulinganifu wa viambishi kati ya Kipemba na lahaja Sanifu (Kiswahili Sanifu). Abdulla (2016) amechunguza kuhusiana na viambishi njeo na hali vya Kipemba huku akijikita kwenye mofofonolojia ya virai vitenzi hasa kwenye

kuangalia tofauti ya midhihiriko na athari zake kwenye muundo ndani na muundo nje. Waandishi wengine ambao wameeleza dhana ya viambishi njeo ni Habwe na Karanja (2004) hao wamefafanua kuwa kiambishi njeo ni mofuinayo wakilisha mofimu ya wakati katika lugha mahsusi.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Tafiti mbali mbali zimekwishafanywa zikiwa na shabaha ya kuchunguza viambishi njeo katika lahaja tofauti. Miongoni mwa kazi hizo ni ile ya Mazrui (1983) aliyechunguza tofauti za mofimu zinazowakilisha njeo katika lahaja ya Mvita, Amu na Unguja na aligundua kwamba kuwepo maumbo ya mofu ambayo yanawakilisha njeo katika lahaja hizo yanapelekea kujitokeza tofauti ya maumbo nje ya kimofolojia. Maganga (1995) yeye alitafiti ulinganishi kati ya lahaja za visiwani (Kiswahili, Kiamakunduchi, Kipemba na Kitumbatu) kwa kuangazia vipengele vya mofofonolojia katika lahaja tofafauti ila mtafiti wa utafiti huu yeye aliangazia lahaja maja tu ya Kitumbatu.. Kuhusu lahaja ya Kipemba Hamad (2011) ingawa alifanya utafiti uliolinganisha kati ya Kipemba na Kiswahili Sanifu lakini hakujihisisha na mofosintaksia ya lahaja hizo. Barno (2013) aliwahi Kufanya utafiti wa muundo wa mofosintaksia katika kikundi tenzi cha Kinandi lakini utafiti wake ulihusu lugha nyingine na sio Kiswahili na lahaja zake. Abdulla (2016) alichunguza viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba bila kuweka wazi midhihiriko ya Kimofosintaksia. Pamoja na jitihada zote zilizofanywa na watafiti waliotangulia mtafiti wa kazi hii hajaona mahali ambapo utafiti kuhusu kimofofolojia ya njeo na hali katika Kitumbatu umefanywa peke yake, watafiti waliotangulia waliangazia katika lahaja nyengine au walichanganya lahaja ya Kitumbatu na lahaja nyengine

kama vile Kimakunduchi, Kipemba, na Kiswahili sanifu (KS). Pia viiambishi njeo ni mofu ambazo huwakilisha mofimu za wakati katika lugha mahsusi. Kila lugha ina mfumo wake wa kuhudhurisha viambishi vyake vya wakati. Kwa muktadha huu mtafiti ameamua kufanya stadu tafiti unaohusiana na uchunguzi wa kimofofonolojia wa viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu ili kupunguza mwanya ulioachwa na watangulizi wake.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

i) Kubainisha viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu.

ii) Kuchanganua athari za kimofofonolojia zinazojitokeza katika vitenzi vya Kitumbatu wakati wa kudhihirisha viambishi njeo na hali.

### 1.4.3 Maswali ya Utafiti

i) Ni Vipi viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu?

ii) Ni athari zipi za kimofofonolojia zinazojitokeza katika lahaja ya Kitumbatu?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Baada ya kukamilika kwake utafiti huu unatazamiwa kuwa ni miongoni mwa marejeo ya kimaktaba yatakayowawezesha walimu, wanafunzi na wadau wengine wa kitaaluma kupata fursa ya kwenda kuusoma na kutambua baadhi ya vipengele

vya kiisimu vinavyohusu lahaja ya Kitumbatu. Pili utafiti huu utakuwa ni kama marejeo ya kidarasa, yatakayowasaidia walimu katika kufundisha na wanafunzi katika kujifunza. Tatu, matarajio ya mtafiti ni kuwa utafiti huu utawashawishi wanaisimu wa kileo kufanya tafiti nyingine ambazo zitahusiana na maswali ya kiisimu yanayohusu viambishi njeo na hali katika lahaja ya nyingine za Kiswahili. Nne, kazi hii itakuwa na umuhiumu mkubwa kwa wanajamii wa Kitumbatu kwa kuwa itakuwa ni kumbukumbu inayoonesha ustawi na uhai wa lahaja za Kiswahili, Kitumbatu ikiwa ni moja wapo.

## 1 .6 Mipaka ya Utafiti

Mtafiti alijipanga kushughulikia kile alichokikusudia tu katika utafiti wake ambacho ni Kuchunguza Viambishi Njeo na Hali katika Lahaja ya Kitumbatu. Mtafiti ameamua kuchunguza viambishi njeo na hali katika lahaja hii kwa sababu vinakaribiana na maumbo ambayo yanaathiriana sana katika lahaja hiyo.Viambishi njeo vitakavochunguzwa ni viambishi vinavyoonesha wakatiuliopo, wakati unaokuja na wakati uliopita. Kwa upande wa viambishi hali, mtafiti alichunguzahali ya mazoea, hali ya sharti na hali ya kuendelea kwa tendo. Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa vipengele hivyo katika Kitumbatu tu na sio katika lahaja nyingine. Pia ulihusu viambishi vilivyotajwa tu na sio viambishi vya aina nyingine.

## 1.7 Changamoto za Utafiti

Changamoto ambazo mtafiti alikutana nazo ni ugumu uliojitokeza katika urejeshaji wa hojaji zilizopelekwa kwa watafitiwa. Watafitiwa wengi hawakurejesha dodoso walizopelekewa, hivyo kuzifanya data kuwa na upungufu jambo ambalo liliyafanya malengo ya utafiti kufikiwa kwa shida. Changamoto hii ilitatuliwa kwa kuzifuata

hojaji hizo kwenye maskani ambako watafitiwa wanaishi na kuzikusanya. Pale ambapo dodoso hizo zilikuwa zimetupwa mtafiti alitoa nyingine na kuzisimamia mpaka zikajazwa na kuondoka nazo. Pili wakati mbinu ya usaili inatumika kulijitokeza changamoto ya hali ya aibu miongoni mwa watafitiwa. Mtafiti aliwaelimisha watafitiwa lengo la utafiti wake na baadae waliyaelewa malengo na kupunguza aibu na hivyo kukubali kuhojiwa.

## 1.8 Mpanglio wa Utafiti

Utafiti huu umeundwa katika sura tano. Sura ya kwanza ni ya utangulizi, kazi yake kuu ni kubanisha vipengelevya awali vinavyogusia kuhusu usuli na tatizo la utafiti. Mambo mengine yaliyobainishwa hapo ni malengo ya utafiti, umuhimu, mipaka ya utafiti pamoja na changamoto za utafiti. Sura ya pili ya utafiti imeonesha fasili ya lahaja, dhana ya mofonolojia pamoja na dhana ya njeo na hali. Sura hii pia imeorodhesha kazi tangulizi ambazo mtafiti alipata fursa ya kuzipitia na kudondoa vipengele vilivyohitajika na vilivochangia katika utafiti huu.Vile vile kiunzi cha nadharia kiliteliuwa kama muongozo wa utafiti.

Sura ya tatu imewasilisha njia na mbinu za utafiti ambazo zimetumika katika kufanya utafiti huu, Sura ya nne ilihusu uchambuzi na uchanganuzi wa data za tutafiti. Utafiti huu ulichambuliwa kwa njia ya maelezo, majedwali yalitumika kuwasilishia data ili kurahisisha uchambuzi. Sura ya tano ilibainisha muhtasari na mapendekezo ya utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii iilihusu machapisho na kazi tangulizi mbali mbali ambazo zimefanana na kukaribiana na mada inayotafitiwa ikiwemo fasili ya lahaja, lahaja ya Kitumbatu, dhana ya mofolojia, dhana ya mofofonolojia, dhana ya kiambishi, viambishi njeo vya Kiswahili, dhana ya hali, kazi tangulizi, kiunzi cha nadharia ambacho kimemuongoza mtafiti katika kukamilisha kazi yake pamoja na muhtasari wa sura hii.

## 2.2 Fasili ya Lahaja

Kwa mujibu wa John na Mduda (2011) lahaja ni vilugha ambavyo vina chimbuko moja, hivyo vinafanana kwa kiasi kikubwa katika vipengele mbali mbali vya kilugha kama matamshi, msamiati, maana na miundo ya tungo Sulhiya (2010) anasema kwamba lahaja ni vilugha mbali mbali vinavyojitokeza kwenye lugha kuu kama vile Kiswahili sanifu. Ali (2016) anasema lahaja ni vilugha vidogo vidogo vya lahaja moja ambayo hubainika kijamii au kijografia na kudhihirishwa na vipengele mbali mbali vya kiisimu kama vile matamshi, miundo ya maneno na misamiati. Hivyo basi, lahaja ni tofauti zilizomo ndani ya lugha kuu moja ambapo watumiaji wa lahaja ya sehemu moja hutofautiana na sehemu nyingine. Mfano lahaja ya kusini Pemba na kaskazini Pemba hutofautiana kidogo kiuzungumzaji kama inavyooneshwa hapo chini.

**Jedwali Na.2.1 Tofauti ya lahaja ya Kusini Pemba na Kaskazini Pemba**

| Kusini Pemba | Kaskazini Pemba |
|---|---|
| Sitaki | Sebu |
| Ondoka | Uka |
| mikate yapo | Mikate ipo |
| Jiwe | Iwe |
| Anguka | Kugwa |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)**

## 2.3 Lahaja ya Kitumbatu

Lahaja ya Kitumbatu ni Kiswahili kinachozungumzwa Tumbatu na Utumbatuni maeneo yanayozunguka kisiwa hicho. Pia lahaja hii huzungumzwa na wakaazi wa kijiji cha Mwambekilichoko Wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba. Lahaja hii pia huzungumzwa sehemu yakusini kisiwani Pemba (Bakari, 2015).

## 2.4 Dhana ya Mofolojia

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2012) mofolojia ni sarufi inalojishughulisha na uchambuzi wa mfumo wa maneno katika lugha. Habwe na Karanja (1999) wamekuja na maoni yanayoenda sambamba na yale ya Massamba na wenzake. Utanzu huu huchunguza sheria au kanuni zinazofuatwa katika kuyapanga maneno ili yalete maana inayokubalika na kuelewaeka katika lugha husika.

## 2.5 Dhana ya Mofofonolojia

Mofofonolojia kwa mujibu wa Massamba (1996) ni tawi la isimu linalohusu mchakato wa kimuingiliano kati ya fonolojia na mofolojia. Mofofonolojia zaidi

hujihusisha na vipengele vya fonolojia ndani ya maumbo ya mofolojia. Mchakato huu hufanyika kupitia kanuni mbalimbali za kifonolojia kama vile uyeyushaji, ukaakaishaji, udondoshaji na kanuni nyenginezo.

### 2.6 Dhana ya Kiambishi

Mgullu (1999) anasema kwamba kiambishi ni istilah ambayo hutumiwa hasa katika uwanja wa mofolojia kueleza sehemu mbalimbali za maneno au mofu ambayo huongezewa (huambishwa). Kihore na wenzake (2003) wanasema kuwa kiambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbali mbali zinazofungamana na neno pamoja na mofimu hizo. Kihore na wenzake (2003) wanaeleza kuwa viambishi katika lugha ya Kiswahili hujitokeza tu mwanzoni au mwishoni mwa mzizi. Habwe na Karanja (2004) wamechambua viambishi vinavyowekwa mwanzoni mwa mzizi huitwa viambishi awali na ambavyo huwekwa katikati huitwa viambishi kati na vile vinavyowekwa mwishoni mwa mzizi huitwa viambishi vifuatilizi. Kwa ujumla maelezo ya wataalamu yanatufahamisha kwamba viambishi ni mofimu zinazopachikwa nyuma au mbele ya mzizi wa neno ili kubadilisha dhana ya neno. Mofimu hizo hupachikwa sehemu mbili tofauti. Tunapata aina mbili za viambishi kwa mujibu wa nafasi zake katika neno yaani viambishi awali ambavyo hupachikwa mwanzoni au nyuma ya mzizi wa neno na viambishi tamati ambavyo hivi hupachikwa mbele au mwishoni mwa mzizi wa neno. Viambishi ni mofimu ambazo hupachikwa mwanzoni au mwashoni mwa mzizi kwa ajili ya kupata maneno mapya.

## 2.7 Dhana ya Njeo

Abdulla (2016) ameielezea njeo kuwa ni kategoria ya kisarufi ambayo huwakilisha muda au wakati ambao tendo hufanyika.Anendelea kufafanua kuwa njeo hueleza uhusiano uliopo baina ya wakati wa kutaka na wakutenda. Anamalizia kwa kusema njeo katika Kiswahili huelezwa na kitenzi. TUKI (1990) wanasema njeo katika Kiswahili hutumika wakati ambapo tendo lilitendeka au halikutendeka. Njeo katika Kiswahili zimegawanyika katika nyakati tatu wakati uliopo, wakati uliopita na wakati unaokuja.

## 2.8 Dhana ya Kiambishi Njeo

Kiambishi njeo ni mofu ambayo huwakilisha mofimu ya wakati katika lugha mahsusi. Kila lugha inategemea mfumo wake wa kuhudhurisha kiambishi chake cha wakati kwa namna inayotofautiana na lugha nyingine. Katika lugha ya Kiswahili kiambishi njeo huja baada ya kiambishi nafsi kabla ya mzizi wa neno. Habwe na Karanja (2004) wamekielezea kiambishi njeo kuwa ni mofu inayowakilisha mofimu ya wakati. Mgullu (1999) amekiita kiambishi hiki kuwa ni mofimu ya njeo. Utafiti huu utaonesha kwamba kiambishi njeo ni mofu inayowakilisha wakati ama uliopo, uliopita au unaokuja.

## 2.9 Viambishi Njeo vya Kiswahili

Katika lugha ya Kiswahili vitenzi ndio huwa na kawaida ya kubeba mofimu ya njeo. Na huja kabla ya mzizi wa kitenzi. Hii ina maana kwamba njeo ni kiambishi awali. Kihore na wenzake waliziorodhesha njeo za Kiswahili kama ifuatavo:-

**Jedwali Na.2.2 Vambishi Njeo vya Kiswahili**

| **Njeo** | **Mfano wa kiambishi** | **Kitenzi** | **Mtindo wa kitenzi** |
|---|---|---|---|
| wakati uliopo | -na- | Unasema | Kukubali |
| Wakati uliopo | -i- | Hatulii | Kukanusha |
| Wakati uliopita | -li- | Alikula | Kukubali |
| Wakati uliopita | -ha- | hakula | Kukanusha |
| Wakati ujao | -ta- | Atakuja | Kukubali |
| Wakati uliopita hali timilifu | -me- | Amerudi | Kukubali |
| Hali ya mazoea | -hu- | Humsaidia | Kukubali |

**Chanzo: Kihore na wenzake (2003)**

## 2.10 Dhana ya Hali

Barno (2013) akimnukuu Comrie (1975) anasema hali ni mtazamo wa vipashio vya ndani vya wakati na jinsi ya tendo linavofanyika, anaeleza kuwa hali inatoa njia tofauti ya kuchanganua vipashio vya ndani vya tendo kwa mfano, swali litakaloulizwa ni lini tendo lilitendeka wakati gani? Lilifanyikaje? Na je! Tendo limekamilika au bado? Comrie (keshatajwa) alitofautisha kati ya njeo na hali anaeleza kuwa njeo huhusu wakati wa hali inayorejelewa na hali ni jinsi ya kuueleza vipashio tofauti vya ndani vya wakati. Kwa mujibu wa Betty (2008) hali ni kuangalia jinsi kitenzi husika kinavyotendeka.

## 2.11 Kazi Tangulizi

Kazi tangulizi alizozipitia mtafiti ni zile ambazo zinahusu lahaja, njeo na hali. Licha ya kazi hizo mtafiti aliangazia kazi zilizohusu tofauti kati ya lahaja mbali mbali na Kiswahili sanifu (KS), ulinganishi wa kiisimu kati ya lahaja ya Kipemba na Kitumbatu, muundo wa kimofosintaksia wa kitenzi cha Kinandi na kazi nyingine zisizokuwa hizo. Ili kuona ni jinsi gani wataalamu mbali mbali wamefanya uchunguzi wa viambishi njeo. Mazurui (1983) amefanya uchunguzi wa vipashio vya njeo za nyakati ya lahaja za Mvita, Bajuni, Amu na Unguja. Juma (2011) alifanya utafiti kuhusu tofauti za kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili cha Wete Pemba. Hamad (keshatajwa) alibaini kuwa kuna muachano mkubwa wa kimofolijia baina ya Ki-Micheweni na Ki-Wete kwa sababu Ki-Micheweni kwa kiasi kikubwa kimehifadhi lahaja yake na Ki-Wete kimepokea mabadiliko makubwa.Utafiti waHamad (keshatajwa) ni muhimu kwa mtafiti, kwani umemsaidia mtafiti kuweza kuona tofauti zenye kuonesha nyakati mbali mbali katika hali ya uyakinishi na haliya ukanushi.

Barno [2013], aliwahi Kufanya utafiti wa muundo wa mofosintaksia katika kikundi tenzi cha Kinandi, alibaini katika utafiti wake kuwa mofosintaksia ya Kinandi, kipatanishi kiima ni cha lazima na huchomoza katika kila tungo, katika sehemu ya kiamilifu ***kptk***[1]ni cha hiari. Pia amebaini kuwa tabia ya kipatanishi kiima si ya thabiti kwa sababu kibainishi chake hubadili nafasi kulingana na muktadha na mada ya matumizi. Utafiti wake ni muhimu kwani umekuwa ni mwanga madhubutiwa kumpa nuru mtafiti katika kutafuta kilchojificha. Pia utafiti wake umekuwa ni msaada mkubwa kwa mtafiti kwani utafiti huu ulimsaidia kuchambua

mofofonolojia ya lahaja ya Kitumbatu kwa kumulika katika mofosintaksia ya Kinandi.

Abdulla (2016) alifanya uchunguzi wa viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba. Alibaini kuwa kuna tofauti baina ya viambishi vinavyowakilisha njeo mbali mbali za nyakati baina ya lahaja za Kipemba, aliona kuwa njeo inayowakilisha wakati uliopita katika Kipemba ni –e- uyakinishi na ukanushi ilhali hali timilifu huwa inawakilishwa na (-n(a-)) katika uyakinishi na ukanushi unawakilishwa na kiambishi {–ja-}.Utafiti wa Abdalla ni muhimu kwani umekuwa ni mwanga ulioomuongoza mtafiti katika kuchambua vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu.

Hamad (2011) alichunguza viambishi njeo na hali kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu (KS).  Hamad (keshatajwa) aliangalia njeo za nyakati zote tatu, wakati uliopo, uliopita na ujao. Pia hakuacha kuangalia hali mbali mbali zinazo jitokeza katika vitenzi, aligundua kuwa viambishi njeo vya Kipemba vinaachana sana na viambishi njeo vya Kiswahili Sanifu (KS).

Habwe na Karanja (2004) walibaini kuwa kiambishi njeo ni kiambishi kinachowakilisha mofimu ya wakati katika lugha mahususi na wamebaini kuwa kuna njeo ya wakati uliopo, wakati uliopita na wakati ujao. Kiujumala tafiti zote hizi zimemsaidia mtafiti kuona viambishi njeo na hali katika lahaja mbali mbali jinsi zinavotofautiana na kukubaliana na Kiswahili sanifu (KS). Hivyo, zinamuonesha mtafiti njia ya kuchunguza viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumabatu.

Masamba na wenzake (1997) wameona kuwa kiambishi njeo ni mofimu ya wakati na wamegundua njeo inayotumika katika lahaja ya Kipemba inatofautiana na Kiswahili Sanifu (KS). Barno (keshatajwa) amesema kuwa njeo ni kategoria ya kimofosintaksia ambayo huwakilisha uhusiano kati ya wakati wa tendo na wakati wa urejelezi ama wakati wa mazungumzo, ameona kuwa njeo inaweza kuwa na uhusiano wa mada na wakati wa matamshi.Vile vile ameelezea kuwa njeo ni kiunganishi cha tukio na ni kategoria amilifu ya kisintaksia. Utafiti waBarno (keshatajwa) umempa mwanga mtafiti kuona jinsi ya kuchambua viambishi njeo na hali katika eneo analolifanyia kazi. Abdulla (2016) akimuelezea Hamad (2011) anasema, katika kazi ya Hamad iliyochunguza tofauti ya viambishia njeo na hali katika lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu (KS) aliangalia njeo za aina zote tatu: njeo ya wakati uliopo, wakati ujao na wakati uliopita. Pia aliangalia viambishi vinavyoangazia hali mbali mbali, alibaini kuwa viambishi njeo vya Kiswahili Sanifu (KS) vinaachana sana na vile vya lahaja ya Kipemba, aliorodhesha tofauti viambishi njeo kati ya Kipemba na Kiswahili Sanifu (KS) kama alivyoviorodhesha katika jaduwali lifuatalo:-

**Jedali Na.2.3 Tofauti ya Viambishio Njeo na Hali baina ya Kipemba na Kiswahili Sanifu (KS)**

| **Kiambishi njeo cha wakati hhali** | **Kiswahili** | | **Kipemba** | |
|---|---|---|---|---|
| Wakati uliopita | -li- | -ku- | -e- | -e- |
| Wakati timilifu | -me- | -ja- | -n-(a)- | -ja-- |
| Ujao | -ta- | -ta- | -ta- | -ta- |
| Wakati uliopo | -na- | -z(+)-(i) | -a- | -z-+(-i) |
| Hali ya sharti | -ki- | -sipo- | -ki- | -sipo- |
| Hali ya kuendelea kwa tendo | -ki- | - | -ki- | -- |
| Kudadisi kwa tendo | Nge | -nge- | -enge- | -senge- |

**Chanzo: Hamad (2011)**

Kazi ya Abdulla (keshatajwa) imempa muelekeo mtafiti kuona jinsi Kiswahili Sanifu (KS) na lahaja zake vinavyoweza kulingana na kutofautiana. Maganga alifanya utafiti unaohusu lahaja za visiwani, alichunguza lahaja ya Kimakunduchi, Kitumbatu, Kipemba na Kiswahli Sanifu (KS). Kazi yake pia ilichunguza viambishi njeo na aligundua kuwepo katika lahaja zote nne njeo za wakati uliopo, unaokuja na uliopita, aligundua hali timilifu, mazoea na hali ya kudadisi kwa tendo, alibaini kuwa kuna tofauti kati ya lahaja ya Kitumbatu, Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu (KS). Mtafiti aligundua kuwa kiambishi njeo {z+--------[i]} ni kwa wakati uliopita yakinishi na (-e-) ni kwa wakati uliopita ukanushi. Aligundua pia lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu hutumia kiambishi -ma-, kuwakilisha wakati timilifu yakinishi na kimbishi -ja- hutumika kwa wakati uliopita ukanushi katika lahaja hizo

(Kimakunduchi na Kitumbatu). Wakati kiambishi -na- hutumika kwa wakati uliopo na uliopita kwa lahaja zote mbili. Katika lahaja hizo wakati ujao hutumia kiambishi -ta- kwa hali ya uyakinishi na ukanushi. Katika hali ya kuendelea kwa tendo na ushuruti katika lahaja ya Kipemba na Kimakunduchi mtafiti amegundua kuwa kiambishi –ka- hutumika. Masamba alionesha viambishi njeo kama vilivyodokezwa katika jedwali (2:1). Jedwali lifuatalo hapo chini Massamba na wenzake (2009) walibainisha njeo za nyakati mbali mbali katika Kiswahili Sanifu (SK).

**Jedwali Na. 2:4 Njeo Za Nyakati Mbali Mbali Katika Kiswahili Sanifu**

| **Kiambishi njeo** | **Uyakinishi** | **Uka nushi** |
|---|---|---|
| Waklati uliopo | -na- | -z+(-i) |
| Wakati ujao | -ta- | -ta- |
| Wakati timilifu | -me- | -ja- |
| Wakati uliopita | -li- | -ku- |
| Hali ya sharti na kuendelea kwa tendo | -ki- | - |
| Hali ya kudadisi kwa tendo | -nge- | -sing- |
| Hali ya kuwa kwa tendo | -li- | -si- |
| Hali ya mfululizo | -ka- | - |

**Chanzo: Massamba na Wenzake (2009)**

Kwa ujumla tafiti zote hizi zilimsaidia mtafiti kuona jinsi viambishi njeo na hali katika lahaja mbali mbali zinavotofaoutiana na kukubaliana na Kiswahili sanifu,

hivyo zilimuonesha njia mtafiti kuchunguza viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu.

## 2.12 Kiunzi cha Nadharia

Kama ilivyoelezwa na Massamba (2004) kuwa nadharia ni mwongozo. Huyo huyo Massamaba akiwa na wenzake (2009) wanasema kuwa nadharia ni utaratibu, kanuni na misingi ya mawazo kwa madhumuni ya kigezo cha kuelezea jambo au mambo kadhaa. Hivyo basi, utafiti huu pia ulihitaji kuongozwa na nadharia inayoendana na mada husika. Kwa hiyo mtafiti alitumia nadharia ya "mofofonolojia" iliyoasisiwa na baba wa surufi zalishi Nikolaj Trubetzkoy(1929 katika mkutano mkuu wa kwanza wa wanafilolojia wa Ki-slavu ambao ulifanyika Prague mwaka 1929. Trubetzkoy alilitumia neno mofofonolojia kwa maana ya tawi la isimu litakaloshughulikia matumizi ya mofolojia katika kufafanua tofauti fulani za kifonolojia.Vile vile nadharia hii ilitumiwa na Bloomfield (1930) akitumia msamiati wa "Mofofonimiki" ikiwa na maana sawa na nadharia ya mofofonolojia ya Trubetzkoy ambayo ilifanya kazi ya kuchunguza mabadiliko ya sauti kwa mahitajio ya kimofolojia katika isimu ya Kimarekani. Kwa mujibu wa Trubetzkoy, mofofonolojia ina kazi zifuatazo:-

Kuchunguza muundo wa mofimu katika lugha, kuchunguza mabadiliko ya sauti yanayotokea mofimu zikiungana, kuchunguza ubadilishanaji wa sauti ambao una uamilifu wa kimofolojia.

Kutokana na dhima za nadharia hii mtafiti ameona kuwa ni nadharia bora iliyoongoza utafiti huu kutokana na uwiyano wake na malengo mahsusi ya utafiti huu. Kazi kuu ya mtafiti katika utafiti huu ni kuchunguza viambishi njeo na hali

katika lahaja ya Kitumbatu na kubaini mabadiliko ya kimofofonolojia yanavyoathiri kiambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu ambayo ndiyo dhima ya nadharia hii.

## 2.13 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii ambayo ni moja katika tano za utafiti mambo mbali mbali yaliweza kuelezewa, mtafiti alianza na utangulizi wa sura, akaelezea kazi mbali mbali ambazozinaelezea viambishi njeo na hali, sura ilimalizia na mkabala wa kinadharia ambao mtafiti aliutumia katika utafiti wake.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Kothari (2004) ameeleza kwamba, mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mbinu hizi zinajumuisha zile mbinuu zote zinazotumika katika kukusanya data. Katika sura hii mtafiti alibainisha eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, aina ya data, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, watoa taarifa na namna matokeo ya utafiti yalivyowasilishwa.

## 3.2 Mkabala wa Kiutafiti

Kwa mujibu wa Kothari (2004) aina ya utafiti ni mpangilio unaomuwezesha mtafiti kupanga utaratibu wa kukusanya na kuchambua data katika kiwango kizuri ambapo pia unajumuisha upatikanaji wa data za uhakika zinazoendana na malengo ya utafiti. Mtafiti katika kazi hii alitumia muundo wa maelezo. Ametumia mkabala huu kwa kuwa katika tafiti za lugha kinachozingatiwa zaidi ni ukweli na uhalisia na sio idadi ya waliokiri au kulikataa jambo. Kwa muktadha huo hoja zilitosha kuelezwa kwa maelezo kuliko kwa kutumia takwimu.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Licha ya kuwa utafiti huu unahusu kuchunguza vismbishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu ila haukufanyika katika kisiwa cha Tmbatu na badala yake ulifanyika kisiwani Pemba, Mkoa wa kusini katika Wlaya ya Mkoani kwenye jimbo la Kangani shehiya ya Mwambe pamoja na shehiya ya Jombwe. Maeneo haya yalichaguliwa kutoka na mtafiti kuona kuwa kuna wazungumzaji wengi wanaozungumza lahaja ya

Kitumbatu ambao walimsaidia kukusanya data zinazohusu viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu.

## 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Kwa mujibu wa Kothari (2004), sampuli ni watafitiwa ambao wameteuliwa kutoka katika kundi kubwa ili watumike katika utafiti. Watafitiwa hao huweza kuwa watu au vitu ambavyo mtafiti ameviteua kwa ajili ya kufanyia utafiti kwa kuzingatia malengo na aina ya utafiti. Cohen na wenzake (2000) wanaeleza kuwa sampuli ni kiwakilishi cha watafitiwa waliokusudiwa kutoa taarifa za utafiti. Sampuli ni seti ndogo ya kundi lengwa ambayo mtafiti atatumia kukusanya taarifa za utafiti wake (Vaeser1998). Baryman (2004) anaeleza kuwani mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi zima. Suwed (2013) anasema kuwa uteuzi wa sampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kutumika katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Katika utafii huu haikuwa kazi rahisi kuhusisha wazungumzaji pamoja na wataalamu wa lahaja ya Kitumbatu, zipo mbinu aina kwa aina za kuchagua sampuli ila mtafiti wa utafiti huu alitumia mbinu ya sampulishaji tajwa (snow ball sampling) ambapo mtafiti aliteua watu hamsini (50) wanaopatikana kwa urahisi na wenye vigezo vya kushiriki katika utafiti na wao walipendekeza wengine zaidi wenye vigezo.

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) usampulishaji ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi huteua kulenga kundi la watu ambao anaamini kuwa ni rasilimali anayotegemea katika utafiti wake. Hivyo mtafiti alitoa uhuru wa wanashehia kushiriki kwa kutoa nafasi kwa wale waliochaguliwa na mtafiti kuchagua wenzi wao

wa karibu waweze kushiriki kutokana na njia hii mtafiti aliweza kurahisisha utafiti wake kwa kuweza kuwafikia watafitiwa wake kiurahisi. Watafitiwa thalathini (30) wa shehiya ya Mwambe na watafitiwa ishirini (20) wa shehiya ya Jombwe, shehiya ya Mwambe katika skuli ya Muambe mtafiti ameweka watafitiwa 30, hii ni kwasababu alishirikisha wasomi ambao ni pamoja na waalimu na wanafunzi, pamoja walioishi hapo kwa muda mrefu ima kwa ukaazi au kuhamia.

**Jedwali Na.3.1 Watoa Taariafa**

| | **Wanawake** | **Wanaume** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| **Shehiya ya Mwambe** | | | |
| Waalimu | 7 | 3 | 10 |
| Wanafunzi | 4 | 4 | 8 |
| Wazee na wakaazi | 7 | 5 | 12 |
| **Shehia ya Jombwe** | | | |
| Wazee na wakaazi | 12 | 8 | 20 |
| Jumla | 30 | 20 | 50 |

**Chanzo: kutoka kwa Mtafiti (2018)**

### 3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Utafiti huu ulitumia data za msingi ambazo mtafiti alizipata kwa kutumia njia mbali mbali. Mbinu au njia za kukusanya data ni mbinu ambazo mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti Kothari (2004). Mtafiti wa utafiti huu alitumia mbinu za aina tatu, ambazo ni mbinu ya dodoso, mbinu ya uchunguzi makini na mbinu ya usaili.

Mtafiti amechukua uamuzi wa kutumia mbinu hizo hapo juu ili kupata uhakika na uthibiti wa matokeo ya kazi yake.

### 3.51 Dodoso

Kwa mujibu wa Kothari (2004) dodoso ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafiti huandika maswali na kisha kuyapeleka kwa watoa taarifa ili wayajibu na baadae kumrudishia mtafiti yakiwa tayari yameshajibiwa. Adamu na Kamuzora (2008) wanaeleza kuwa Dodoso ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafiti huandika maswali na kisha kuyapeleka kwa watoa taarifa ili wayajibu na baadae kumrudishia mtafiti yakiwa tayari yameshajibiwa. Adamu na Kamazora (2008) wanaeleza kuwa Dodoso ni mbinu ya kukusanya data inayohusisha maswali yalioandaliwa kuhusu mada fulani na kumtaka mtafitiwa kujibu kwa maandishi. Maswali yanayotayarishwa yanawezakuwa yanahitaji majibu mafupi au marefu kulingana na taarifa zinazohitajika, pia kulingana na mtu anayepewa. Abdulla (2016) akimnukuu Wallman (2011) ameeleza kuwa maswali ya dodoso yako ya aina mbili ambapo aina ya kwanza ni ile inayohusu maswali funge ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kutoa jibu miongoni mwa majibu kadhaa yaliyopendekezwa. Dodoso ya aina hii ni rahisi sana kujibu na inasaidia kupata majibu maalumu na husaidia kuepusha upendeleo. Aina ya pili ya dodoso ni ile ya dodoso inayohusisha maswali huru (yasiofunge) ambayo hayotoi fursa kwa watafitiwa kuwa huru kueleza wanachokijua juu ya dhana fulani kutegemeana na kile alichoulizwa aina hii haitoi uhuru kwa watafitiwa kueleza mawazo yao kwa ubainifu na uwazi na wala haisaidii kupata taarifa nyingi zaidi. Mbinu ya dodoso katika utafiti huu ilihusisha maswali funge. Mtafiti alitumia aina hii ya dodoso katika utafiti kwa kuwapatia watafitiwa wake, alitumia maswali ya

aina hii kwa kuamini kuwa ndio ambayo yatampatia majibu ya uhakika, na kwa watafitiwa watakuwa huru na watatoa maelezo bila woga wa aina wowote. Mtafiti alipendekeza kutumia mbinu hii ya dodoso kwa kuona kuwa itamuepushia usumbufu kwa watafitiwa wake kutokana na kuwa ndio maswali yanayoendana na watafitiwa kulingana na kiwango cha elimu hii ni kwa sababu kuwa dodoso ina ubora wake na udhaifu wake.

Ubura wa kutumia mbinu hii ni:-

- Haichukui muda mrefu wa kukusanya data.
- Watafitiwa wako huru kueleza wanachokijua bila pingamizi.
- Pia inasaidia kuepusha upendeleo

Ingawa njia hii ina faida ila hakuna kilikicho na faida kikakosa hasara miongoni mwa hasara zake ni:-

- Wanaoweza kujibu mswali ni wale wanaoweza kusoma na kuandika tu
- Ina gharama, kama vile gharama za uchapaji, ununuaji wa kalamu pamoja na posho kwa watafitiwa
- Upoteaji wa dodoso zilizogawiwa kwa watafitiwa
- Hairuhusu maswali ya papo kwa papo
- Ni rahisi kwa watafitwa kupeana majibu.

Mtafiti wa utafiti huu aligawa dodoso zake kwa watafitiwa wake ambao ni waalimu na wanafunzi wa skuli wa muambe.

### 3.5.2 Uchunguzi Makini

Uchunguzi makini ni mbinu ya kukusanya data inayohusiana na tabia za watu, vitu na matukio katika mpangilio maalumu. Chanzo cha uchunguzi makini katika utafiti huu ilikuwa ni wa uwandani kwa kurekodi na kuandika majibu ya hojaji ambazoziliitayarishwa kwa ajili ya kuwauliza watafitiwa wake. Uchunguzi makini umeainishwa katika aina mbili, aina ya kwanza ni uchunguzi makini unaothibitiwa, uchunguzi huu hupatikana kutokana kwa kupitia vitu vilivyowekwa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na aina ya pili ni uchunguzi makini usio na udhibiti, uchunguzi makini wa aina hii hupatikana sehemu za maumbile halisi na hupatikana kwa kutumia dhana za uchunguzaji (Kothari 2004) mtafiti alitumia mbinu hii ili kupata data za uhakika zenye kuaminika na kupunguza dosari. Kutokana na njia hii ya uchunguzi makini, alitumia mbinu hii ya uchunguzi makini ya udhibiti, kwa ajili ya kupata data za awali mtafiti hakutumia njia ya uchunguzi makini isio ya uthibiti kwani isingempatia data za awali kwa wazungumzaji wa asili wa lahaja ya Kitumbatu. Willman (keshatajwa) anasema kwamba data za awali ni data zinazoaminika kwa sababu zinapatikana au kurekodiwa moja kwa moja kutoka kwenye tukio, mtafiti wa utafiti huu alitumia mbinu ya uchunguzi makini wa kudhibiti matukio kwa kwenda katika eneo la utafiti na kutafuta watafitiwa ambao aliwafanyia utafiti katika eneo hilo na kuweza kupata data za uhakika.

### 3.5. 3 Mbinu ya Usaili

Kwa mujibu wa Kothari (2004) mbinu hii ilimsaidia mtafiti kuweka bayana istilahi ambazo hazieleweki kwa watu walioulizwa, mbinu hii ilimuwezesha mtafiti kupata taarifa za ziada na za kina. Anaelezea kuwa ilimruhusu mtafiti kuulizwa maswali ya

ziada na pia kumuwezesha kuwa karibu na watoa taarifa mbinu hii ilihusisha mkusanyiko wa maswali kwa watafitiwa na kujibiwa ana kwa ana. Wasailiwa thalathini na mbili (22) watatafitiwa wakiwemo wanawake kumi (11) na wanaume (11)

Njia hii ina faida nyingi miongoni mwa faida hizo ni:-

i) Ni njia mzuri kwa watafitiwa wote wanaojua kusoma na wasiojua kusoma
ii) Ni njia inayotoa uhuru kwa mtafitiwa kujieleza kwa mapana zaidi na pia inaruhusu kufafanua yale yasioeleweka vyema kwa watafitiwa na kuweza kurekebisha majibu kwa kadri ya uhitaji wa matafiti.
iii) Humuwezesha mtafiti kupata data anazozihitaji kwa haraka zaidi

Njia hii pia ina hasara zake ambapo miongoni mwazo ni:-

i) Njia hii haito taarifa sahihi juu ya jambo lililopita au lilotokea muda mrefu.
ii) Ni njia inayotumia muda mwingi kwa hiyo inamfanya mtafiti atumie idadi ndogo ya sampuli
iii) Baadhi ya wakati mtafitiwa anaweza kutoa taarifa zenye upendeleo kwa mtafiti kutokana n a muongozo aliopewa na mafiti.
iv) Njia hii inahitaji mtafiti kuwa na utaalamu, ujuzi na uzoefu katika utekelezaji wake.

Njia hii aliitumia mtafiti kwa kuchagua mtoa taarifa mmoja na kumuomba awchague wenzake ambao anjua kama wanaweza kutoa taarifa.

## 3.6 Mbinu za Kuchambua Data

### 3.6.1 Maana ya Data

Kwa mujibu wa kamusi la BAKIZA (2010) Data ni mkusanyiko wa taarifa za kiuchunguzi wa kitaalamu unaopelekea uhakika wa kupatikana usahihi wa jambo. Bakagila na wenzake (2005) wanasema kwamba data ni habari iliokusanywa kwenye eneo la utafiti. Kamili (2005) anasema data ni habari ambazo kwa kawaida huwekwa kwa kutumia nambari, ambapo data hizo huwa ni za kimaelezo au kitakwimu. Hivyo basi data ni taarifa mbali mbali zinazotolewa baada ya kufanyika uchunguzi wa kitu fulani ima kwa maelezo au kwa nambari

### 3.6.2 Uchambuzi wa Data

Abdulla (2016) akimnukuu Jamali na Kamuzora (2008) na wao wakimnukuu Kothari (2004) Uchambuzi wa data ni mchakato wa kuchanganua taarifa fulani zilizopo ili kupata mpangilio wa mahusiano miongoni mwa makundi mbali mbali ya taarifa zilizo kusanywa. Katika utafiti data huchanganuliwa kwa kutumia mikabala miwili. Mkabala wa kwanza ni wa kimaelezo na mkabala wa pili ni mkabala wa kitakwimu.Williman (2011) mkabala wa kiidadi (kitakwimu) ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data kwa kutumia nambari ili kurikodi taarifa na kuwasilisha kwa kuitumia mbinu za kitakwimu. Enon (1998) anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi (kimaelezo) ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data ambapo mtafiti ataeleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo. Utafiti huu ulizingatia zaidi uchambuzi wa kimaelezo.. Hivyo basi uchambuzi huu ulikuwa bora zaidi kwa mtafiti kuliko ule wa mkabala wa kiidadi kwa kuchambua na kufafanua

data kila atakapohitajika kufanya hivyo. Na hata ilipojitokeza kutumia mkabala wa kiidadi basi mtafiti aliutiumia.

## 3.7 Misingi ya Maadili

Katika kufanikisha utafiti huu mtafiti hana budi kueleza maadili ya utafiti. Kwa mujibu wa Waziri (2016) akimnukuu Seture (2010) mkabala wa maadili ni moja wapo ya masuala muhimu ambayo mtafiti alipaswa kuzingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukukamilisha utafiti wake. Adamu na wenzake wametaja maadili ya utafiti kwamba ni haki ya kuwa na usiri yaani mtafiti hatoi siri. Anafafanua, haki ya mtafitiwa ni kuhakikisha usalama wake, haki ya kujua madhumuni, haki ya kupata matokeo ya utafiti na haki ya kushiriki kwenye utafiti. Abdulla (2016) akimnukuu Mathooko (200:15) ansema misingi ya maadali ya utafiti ni kaida zilizoelekeza tabia zetu katika mahusiano yetu ya kila siku na wenzetu. Katika utafiti huu maadili ni heshima na tabia njema kwa wale ambao tunaelekea kufanya nao utafiti pamoja na uadilifu kwa kinachotafitiwa ili yaweze kuwa manufaa kwa watu wote. Hivyo katika utafiti huu mtafiti atazitambua haki zote za watafitiwa wake na kuzifanyia kazi, ambapo ataweleza watafitiwa kwamba hakuna tatizo na ikibidi kutokea basi mtafiti ndie atakae beba jukumu hilo.

## 3.8 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii matafiti alibainisha mbinu au njia mbali mbali alizotumia katika kukusanya data ambazo ni mbinu ya dodoso, uchunguzi makinuni na mbinu ya usaili, muundo wa utafiti, ukusanyaji wa data na uchambuzi wa data, eneo la utafiti ambalo ni shehia Mwambe na Shehia ya Jongwe, watoa tarifa pamoja na usampuli na usampulishaji pia ukiwemo na msingi wa maadili.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UFAFANUZI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii iliwasilisha na kujadili data za utafiti. Data zilizowasilishwa na kujadiliwa ni zile zilizoakisi malengo mahsusi ya utafiti huu ambayo ni kubainisha viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu na kubainisha athari za kimofofonolojia zinazojitokeza wakati wa kudhihirisha viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu.

## 4.2 Viambishi Njeo katika Lahaja ya Kitumbatu

Sehemu hii ilihusika na kuyaeleza maumbo ya njeo za wakati zinazotumika katika lahaja ya Kitumbatu. Kwa mujibu wa data lahaja ya Kitumbatu ina viambishi njeo kadhaa vifuatavyo: Kiambishi njeo cha wakati uliopita, Kiambishi njeo cha wakati ujao na kiambishi njeo cha wakati uliopo. Pia lahaja ya Kitumbatu ina viambishi vya njeo ambavyo huonesha wakati wa hali ya mazoeya, hali ya sharti ya kutokea kwa tendo, na wakati wa hali ya kudadisi kwa tendo. Uainishaji huu utazingatia hali ya uyakinishi na ukanishi.

**Jedwali na: 4:1 Viambishi Njeo vya Hali ya Uyakinishi na Hali ya Ukanushi katikaLahaja ya Kitumbatu**

| *Njeo* | *Kiambishi* | |
|---|---|---|
| | **Hali ya uyakinishi** | **Hali ya ukanushi** |
| Wakati uliopita | Tangamano la Irabu (Z+----Ti) | -e- |
| wakati uliopo | -na- | -na- |
| wakati ujao | -ta- | -ta- Tangamano la Irabu (Z+----Ti) |
| hali ya ushuruti | -nge-, -ngeli-,+ –ka- | -nge-, ngeli,+ si(po) |
| hali ya mazoea | hu- | tangamano la irabu (Z+----Ti) |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

### 4.2.1 Kiambishi Njeo Kinachowakilisha Wakati Uliopita katika Lahaja ya Kitumbatu katika Kitenzi cha Kawaida

Kwa kutumia mbinu ya dodoso ambayo mtafiti aliitumia katika kukusanya data tarehe 13/12/2017 na ushuhudiaji alioshiriki tarehae 22/12/2017 mtafiti amebaini kwamba kiambishi njeo ambacho huwakilisha wakati uliopita katika uyakinishi ni {**z+----Ti}** katika Kitumbatu. Katika ukanushi njeo ya wakati huo huwakilishwa {**–e-}.**Madai haya yanathibitishwa na data ifuatayo kama inavyoonekana hapo chini. Jedwali la hapo chini linaonesha ni kwa namna gani Kitumbatu kinatumia kiambishi kapa na kufuatiwa na tangamano la irabu katika hali ya uyakinishi na jinsi kinavyotumia kiambishi {-e-} katika hali ya ukanushi. Hapa inaonekana kwamba nadharia ya Mofofonolojia imeakisiwa vizuri sana kwa kuwa imeonesha wazi jinsi viambishi njeo viliivyoainishwa kwenye jedwali na. 4.1 vilivyodhihiri kwenye

vitenzi vilivyo kwenye jedwali na. 4.2. Jambo hili limeonesha jinsi nadharia ya mofofonolojia ilivyotekeleza moja miongoni mwa kazi zake za msingi ambayo ni Kuchunguza muundo wa mofimu katika lugha. Hapa maumbo yanayowakilisha mofimu za njeo za wakati yamewekwa bayana kabisa.

**Jedwali na. 4:2 Jinsi Kiambishi cha Njeo Wakati uliopita Kinavyofanya Kazi**

| **Kitenzi** | **Lahaja ya Kitumbatu** | | **Kiswahili Sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Uyakinishi** | **Ukanushi** | **Uyakinishi** | **Ukanushi** |
| Piga | Nip**igi** | Si**e**piga | nilipiga | Sikupiga |
| Imba | Kaimbi (kemb**i)** | H**e**kwimba | aliimba | hakuimba |
| Cheka | Kach**e**k**e** | ha**e**cheka(hecheka) | alicheka | hakucheka |
| Sema | Kus**e**m**e** | hu**e**sema(hwesema) | ulisema | Hukusem |
| Soma | Nis**o**m**o** | S**e**soma | nilisoma | Sikusoma |
| Oga | Ku**o**g**o** **(**ko**go)** | hu**e**koga(hwekoga) | ulioga | Hukuoga |
| Nuna | Tun**u**n**u** | hatu**e**nuna (hatw**e**nuna) | tulinuna | Hatukununa |
| Fuma | Kuf**u**m**u** | hu**e**fuma (hw**e**fuma) | ulifuma | Hukufuma |
| Fanya | Muf**a**ny**a** | hamuefanya(hamwefanya) | mulifanya | hamukufanya |
| Kata | Wak**a**t**a** | hawa**e**kata (haw**e**kata) | walikata | Hawakukata |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

Kwa ujumla data zinaonesha kuwa Kitumbatu hutumia kiambishi kapa na kufuatiwa na tangamano la irabu {**z+-----Ti}** katika hali ya uyakinishi nahutumia kiambishi {–

e-} katika hali ya ukanushi.Athari za kimofolojia zimejitokeza kwenye vitenzi hivyo katika hali ya uyakinishi na ukanushi.Athari hizi hazitojadiliwa hapa na zitajadiliwa katika lengo la pili la utafiti huu.

### 4.2.2 Kiambishi kinachowakilisha Njeo ya Wakati Ulipita katik Kitezi kilichoanza na Iarbu /i/, /e/, /o/ na irabu /u/ katika Mzizi

Ufuatao ni uwasilishaji wa kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati uliopita kwenye kitenzi kilichoanza na irabu /i/ katika mzizi kama inavyodhihiri kwenye jedwali na 4.3 liliopo hapo chini.

**Jedwali na. 4.3 Viambishi Njeo vinavyowakilisha Wakati uliopita katika Vitezi vilivyoanza na Irabu -/i-/ katika Mzizi**

| Nafsi | Kitenzi | Muundo ndani | Muundo nje | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| **N1 umoja** | Iba | Niibi | nyibi | niliiiba |
| **Wingi** | | Tuibi | twibi | tuliiba |
| **N2 umoja** | Ita | Kuiti | kwiti | uliita |
| **Wingi** | | Muiti | mwiti | muliita |
| **N3 umoja** | Imba | Kaimbi | kembi | aliimba |
| **Wingi** | | Waimbi | wembi | waliimba |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

**Jedweli na. 4.4 Viambishi Njeo Vinavyowakilisha Wakati Uliopita katika Vitenzi vilivyoanza na Irabu /-e-/ katika Mzizi**

| **Nafsi** | **Kitenzi** | **Miundo ndani** | **Miundo nje** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|---|
| **N1 umoja** | enda | Niende | nyende | Nilikwenda |
| **Wingi** | | Tuende | twende | tulienda |
| **N2 umja** | eleza | Nieleze | nyeleze | nilieleza |
| **Wingi** | | Mueleze | mweleze | mulieleze |
| **N3 umoja** | epuka | Kaepuke | kepuku | Aliepuka |
| **Wingi** | | Waepuke | wepuku | Waliepuka |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

**Jedwali Na: 4.5 Viambishi Njeo vinavyowiakilisha Wakati uliopita katika Vitenzi vilivyoanza Irabu /-o-/ katika mzizi**

| **Nafsi** | **Kitenzi** | **Muundo ndani** | **Muundo nje** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|---|
| **N1 umoja** | oga | Niogo | nyogo | Nilioga |
| **Wingi** | | Tuogo | Togo | Tulioga |
| **N2 umoja** | okoa | Kuokoo | kuyokoyo | Tuliokoa |
| **Wingi** | | Muokoo | muyokoyo | Muliokoa |
| **N3 umoja** | ona | Kaono | Kono | Aliona |
| **Wingi** | | Waono | wono | Waliona |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

**Jedwali Na: 4.6 Viambishi Njeo vinavyowakilisha Wakati uliopita vilivyoanza na Irabu /-u-/ katika Mzizi**

| **Nafsi** | **Kitenzi** | **Muundo ndani** | **Muundo nje** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|---|
| **N1 umoja** | unda | Niundu | Niyundu | Niliunda |
| **Wingi** | | Tuundu | Tuyundu | Tuliunda |
| **N2 umoja** | unda | Kuundu | Kuyundu | Uliunda |
| **Wingi** | | Muundu | Muyundu | Muliunda |
| **N3 umoja** | uka | Kauku | Kauku | Aliuka |
| **Wingi** | | Wauku | Wauku | Waliuka |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

**Jedweli Na:4.7 Viambishi njeo vinavyowakilisha Wakati uliopita Vilivyoanza na Irabu /-a -/ katika Mzizi**

| **Nafsi** | **Kitenzi** | **Muundo ndani** | **Muundo nje** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|---|
| **N1 umoja** | acha | Niacha | nyacha | Niliacha |
| **N1 wingi** | | Tuacha | twacha | Tuliacha |
| **N2 omoja** | anza | Kuanza | kwanza | Ulianza |
| **N2 wingi** | | Muanza | mwanza | Mulianza |
| **N3 umoja** | apa | Kaapa | kayapa | Aliapa |
| **N3 wingi** | | Muapa | muyapa | Muliapa |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

Kama ilivyo katika vitenzi vya kawaida, vitenzi vilivyoanza na irabu huchukua kiambishi kapa kinachofuatiwa na tangamano la irabu kuwakilisha njeo ya wakati uliopita muda mrefu. Vitenzi vinavyoanza na irabu /-i-/ vinapoambikwa nafsi za mtenda husababisha mkutaniko wa irabu mbili zinazoibua michakato kadhaa ya kimofofonolojia inayogeuza maumbo ya vitenzi. Kwa mfano, iwapo kitenzi kilichoanza na irabu /-i-/ kitaambikwa nafsi ya kwanza na ya pili umoja na wingi kanuni ya uyeyushaji hujitokeza kama ilivyo kwenye jedwali Na. 4.3. Kitenzi cha aina hiyo kikiambikwa kiambishi nafsi ya tatu umoja na wingi kanuni ya mvuatano wa irabu hujitokeza. Kwa kuthibitisha hili natuangalie kitenzi -imba kwenye jedwali Na. 4.3 hapo juu. [imba]→[ kaimbi}→[kembi].

Iwapo kitenzi cha Kitumbatu kimeanza na irabu /-e-/ na kuambikwa kiambishi nafsi ya kwanza na ya pili umoja na wingi hali inakuwa ni sawa na vile ilivyojitokeza wakati wa uambikaji nafsi ya kwanza na ya pili kwenye kitenzi kilichoanza na irabu /-i-/. Kwa ushahi zaidi angalia jedwali Na. 4.4 kuthibitisha hoja za mtafiti.

Tunapoambika nafsi ya kwanza umoja kwenye kitenzi kilichoanza na irabu /-o-/ uyeyushaji hujitokeza, tukiambika nafsi ya kwanza wingi udondoshaji hujitokeza. Uambikaji wa nafsi ya pili umoja na wingi husababisha uingizwaji wa sauti /–y-/ kuvunja mkutaniko wa irabu mbili ambazo haziruhusiwi kwenye Kitumbatu katika muundo wa nje. Uambikaji wa nafsi ya tatu kwenye kitenzi cha aina hii husababisha udondoshaji. Angalia jedwali Na. 4.5 kuthibitisha hoja iliyotolewa na mtafiti.

Iwapo kitenzi kilichoanza na irabu /-u-/ kitaambikwa nafsi ya kwanza umoja na wingi sauti /-y-/ huingizwa ili kuvuja mkutaniko wa irabu mbili kwenye kitenzi

hicho. Iwapo kiambishi nafsikinachowakilisha nafsi ya tatu umoja kitaambikwa kwenye kitenzi cha aina hii kwenye umoja na wingi kunakuwa hakuna mabadiliko. Mkutaniko wa irabu mbili hapa hujitokeza kama vighairi. Angalia jedwali Na. 4.6 kuthibitisha hoja iliyotolewa na mtafiti.

Iwapo kitenzi kilichoanza na irabu /-a-/ kitaambikwa kiambishi nafsi ya kwanza na ya pili umoja na wingi kwenye Kitumbatu, basi uyeyushaji hujitokeza. Iwapo kiambishi nafsi ya tatu umoja na wingi husababisha uingizwaji wa sauti /–y-/ kuvunja mkutaniko wa irabu mbili ambazo haziruhusiwi kwenye Kitumbatu katika muundo wa nje.

### 4.2.3 Kiambishi kinachowakilkisha Njeo ya Wakati uliopo katika Lahaja ya Kitumbatu

Kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati uliopo kimebainika kwa kutumia mbinu ya dodoso iliyokusanywa tarehe 13/12/2017 na ushuhudiaji tarehe 22/12/2017. Mtafiti amebaini kwamba kiambishi njeo ambacho kinawakilisha wakati uliopo ni {-na-} katika hali ya uyakinishi na ukanushi. Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha jinsi kiambishi {-na-}, kinavyowakilisha njeo ya wakati uliopo.

**Jedwali na. 4.8 kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati uliopo katika Lahaja ya Kitumbatu**

| Kitenzi | Lahaja ya kitumbatu | | kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| | Uyakinishi | Ukanushi | uyakinishi | Ukanushi |
| Soma | tu***na***soma<br>mu***na***soma<br>ka***na***soma | hatu***na***soma<br>hamu***na***soma<br>ha***na***soma | tunasoma<br>munasoma<br>anasoma | hatusomi<br>hamsomi<br>hasomi |
| Imba | tu***na***kwimba<br>m***na***kwimba<br>wa***na***kwimba | ha***tu***nacheza<br>ham***na***kwimba<br>hawa***na***kwimba | tunanaimba<br>munaimba<br>wanaimba | hatuimbi<br>hamukwimbi<br>hawaimbi |
| La | tu***na***kula<br>mu***na***kulya<br>wa***na***kulya | hatu***na***kulya<br>hamu***na***kulya<br>hawa***na***kulya | tunakula<br>munakula<br>wanakula | hatuli<br>hamuli<br>hawali |
| Ja | n***na***kuja<br>ku***na***kuja<br>ka***na***kuja | Si***na***kuja<br>hu***na***kuja<br>ha***na***kuja | Ninakuja<br>unakuja<br>anakuja | Siji<br>huji<br>haji |
| Ruka | n***na***ruka<br>ku***na***ruka<br>ka***na***ruka | si***na***ruka<br>hu***na***ruka<br>ha***na***ruka | Ninaruka<br>unaruka<br>anaruka | Siruki<br>huruki<br>haruki |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

Jedwali Na: 4.8 linaonesha jinsi ambavyo lahaja ya Kitumbatu hutumia kiambishi {-na-} kubainisha njeo ya wakati uliopo katika hali ya uyakinishi na katika hali ya ukanushi. Kiujumla data ambazo zilikusanywa zinaonesha kuwaKitumbatu hutumia kiambishi {-na-} katika hali ya ukanushi na uyakinishi. Athari za kimofofonolojia

zimejitokeza katika vitenzi vinavyoonesha hali ya uknushi. Athari hizo hazitojadiliwa katika lengo hili, na badala yakeziitajadiliwa katika lengo la pili la utafit huu.

### 4.2.4 Kiambishi Njeo kinachowakilisha Wakati Unaokuja katika Lahaja ya Kitumbatu

Katika Kitumbatu kiambishi njeo kinachowakilisha wakati unaokujani {-ta-} katika hali yauyakinishi. Katika ukanushi kiambishi -ta- na muundo kapa unaofatiwa pia. Jedwali (4.1) linaonesha ukwaeli wa hayo aliyoyaashiria mtafiti hapo juu.

**Jedwali Na. 4.9: Kiambishi kinachowaklisha Njeo ya Wakati ujao**

| **Kitenzi** | **Lahaja ya Kitumbatu** | | **Kiswahili Sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Uyakinishi** | **Ukanushi** | **Uyakinishi** | **Ukanushi** |
| Soma | n***ta***soma<br>tu***ta***soma<br>ku***ta***soma<br>m***ta***soma<br>wa***ta***soma | Si***ta***soma<br>hu***ta***soma<br>ham***ta***soma<br>hawa***ta***soma<br>hawa***ta***soma | Nitasoma<br>tutasoma<br>utasoma<br>mutasoma<br>watasoma | sitasoma<br>hatutasoma<br>hutasoma<br>hamutasoma<br>hawatasoma |
| Imba | N***ta***kwimba<br>tu***ta***kwimba<br>ku***ta***kwimba<br>ku***ta***kwimba<br>wa***ta***kwimba | si***ta***kwimba<br>hatu***ta***kwimba<br>hatu***ta***kwimba<br>ham***ta***kwimba<br>hawa***ta***kwimba | nitaimba<br>tutaimba<br>utaimba<br>mutaimba<br>wataimba | Sitaimba<br>hatutaimba<br>hutaimba<br>hamutaimba<br>hawataimba |
| Pata | N***ta***pata<br>tu***ta***pata<br>ku***ta***pata<br>m***ta***pata | Si***ta***pata<br>hatu***ta***pata<br>hu***ta***pata<br>hum***ta***pata | ntapata<br>tutapata<br>utapata<br>mutapata | Sitapata<br>hatutapata<br>hutapata<br>hamutapata |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

Kama inavyoonekana katika jedwali Na (4.9), kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati ujao katika lahaja ya Kitumbatu ni {*-**ta**-*} katika hali ya uyakinishi na ukanushi.Wakati mwengine Watumbatu hutumia kiambishi ***(z+-------Ti)*** *kuwakilisha* wakati ujao kama ilivyo kwa wakati uliopita muda mrefu. Hali hii hujitokeza pale ambapo mtu amepinga jambo ambalo msemaji kwa uoni wake anahisi litafanywa, lakini msikilizaji akapinga kwamba halitofanywa. Data katika jedwali Na. (4.10) inaonesha wazi jinsi kiambishi cha aina hii kinavyotumika.

**Jedwali Na. 4.10: Kiambishi kinachowaklisha Njeo ya Wakati ujao Ukanushi (z+-----------Ti)**

| **Kitumbatu** | | **Kiswahili Sanifu** | |
|---|---|---|---|
| **Kauli ya Msemaji** | **Jibu la Msikilizaji** | **Kauli ya Msemaji** | **Jibu la Msikilizaji** |
| Ukambiwa ku**ta**gomba | Sigomb**o** | ukiambiwa utagomba | Sigombi |
| Ukamona kutacheka | Sicheke | Ukimuona utacheka | Sicheki |
| Wakawambia wa**ta**nuna | Hawanun**u** | wakiwaambia watanuna | Hawanuni |
| Watapiga makelele | Hawapig**i** | Watapiga makekeke | Hawpigi |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

Data hii inaonyesha kwamba kiambishi kinachowakilishi njeo ya wakati ujao kwenye vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu ni umbo kapa linalofatiwa na tangamano la irabu {Φ+--Ti}

### 4.2.5 Kiambishi Kinachowakilisha Haliya Ushuruti katika Lahaja ya Kitumbatu

Kiambishi ambacho kinawakilisha hali ya ushuruti katika lahaja ya Kitumbatu ni {-***nge***-},{-***ngeli***} pamoja na ***{-ka-***} katika uyakinishi. Na katika hali ya ukanushi njeo ya ushuruti huwakilishwa na {-***nge***-} na {-***ngeli-***} inayotanguliwa na kiambishi {***-si-***}. Ukanushi wa umbo ***{-ka-}*** linalowakilishahali ya sharti katika Kitumbatu ni {-***si***po}. Hapa {-si-} ni mofu ya ukanushi, ilhali {-po} ni mofu ya urejeshi.

**Jedwali Na 4.11 (a): Kiambishi –nge- katika Hali ya Ushuruti**

| Kitenzi | Lahaja ya Kitumbatu | | Kiswahili Sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| | uyakinishi | Ukanushi | uyakinishi | Ukanushi |
| Anguka | n***nge***kugwa<br>tu***nge***kugwa<br>ku***nge***kugwa | n***singe***kugwa<br>tu***singe***kugwa<br>u***singe***kgwa | ungeanguka<br>tungeanguka<br>ungeanguka | usingeanguka<br>tusingeanguka<br>usingeanguka |
| Pika | mu***ngeli***pika<br>ka***ngeli***pika<br>wa***nglie***pika | mi***singeli***pika<br>ka***singeli***pika<br>wa***singeli***pika | mungepika<br>angepika<br>wangepika | Msingepika<br>asingepka<br>wasingepika |
| Tazama | n***geli***kyunza<br>tu***ngeli***kyunza<br>ka***nge***kyunza | nsi***ngeli***kyunza<br>tu***singeli***kyunza<br>ka***singe***kyunza | ningetazama<br>ungetazama<br>angetazama | nisingetazama<br>uingetazama<br>asingetazama |
| Rudi | ku***nge***rudi<br>m***nge***rudi<br>ka***nge***rudi<br>wa***nge***rudi | u***singe***rudi<br>m***singe***rudi<br>ka***sing***erudi<br>wa***singe***rudi | ungerudi<br>mungerudi<br>angerudi<br>wangerudi | usingerudi<br>msingerudi<br>asingerudi<br>wangerudi |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

Data iliyopo hapo juu inaonesha kuwa kiambishi kinachowakilisha hali ya sharti kwenye uyakinishi ni {-nge-} na {-ngeli-} na katika ukanushi ni {-singe} na {-singeli-}.Ushuruti -ka- kama ilivyoelezwa hapo juu huwakilishwa na umbo -sipo- kwenye ukanushi wake. Jedwali hapo chini linaonyesha wazi jinsi ukweli huo ulivyodhihirishwa.

**Jedwali Na. 4.11(b) Kiambishi cha Sharti –ka- na Ukanushi wake kinavyodhihiri katika Lahaja ya Kitumbatu**

| Kitenzi | Lahaja ya kitumbatu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| Soma | n***ka***soma<br>tu**ka**soma | n***sipo***soma<br>tu**sipo**soma | nikisoma<br>tukisoma | nisiposoma<br>tusiposoma |
| Lia | a**ka**lia<br>wa**ki**lia | A**sipo**lia<br>Wa**sipo**lia | akilia<br>wakilia | asipolia<br>wasipolia |
| Piga | a**ka**piga<br>wa**ka**piga | A**sipo**piga<br>Wa**sipo**piga | akipiga<br>wakipiga | Asipopiga<br>wasipopiga |
| Cheza | u**ka**cheza | Wa**sipo**cheza | wakicheza | wakicheza |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

### 4.2.6 Kiambishi kinachowakilisha Hali ya Mazoea

Lahaja ya Kitumbatu hutumia kiambishi {-hu-} kuwakilisha hali ya mazowea katika uyakinishi na kiambishi **{z—ti}** kwenye ukanushi. Jedwali namba na. 4.12 linaonesha hali iliyoashiriwa na mtafiti hapo juu:-

**Jedwali Na 4.12 Kiambishi kinachowakilisha Hali ya Mazoea**

| Kitenzi | Lahaja ya Kitumbatu | | Kiswahili Sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| | uyakinishi | Ukanushi | uyakinishi | ukanushi |
| Suwaki | ***miye hu***swaki | ***mie si***suwaki | mie hupiga mswaki | mie sipigi mswaki |
| | ***sue hu***swaki | ***sue ha***tusuwaki | hupiga mswaki | hatupigi mswaki |
| Lala | ***Weye hu***lala mapema | ***hu***lali mapema | hulala mapema | hulali mapema |
| | ***hu***lala mapema | ***ha***mulali mapema | hulala mapema | hamulali mapema |
| Imba | ***huimba (whimba)*** | ***Haimbi*** | Huimba | haimbi |
| | ***hu***kwimba | ***Ha***wakwimbi | Huimba | hawaimbi |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

### 4.2.7 Kimbishi Kinachowakilisha Hali ya Kuendelea kwa Tendo Katika Lahaja ya Kitumbatu

Katika lahaja ya Kitumbatu kiambishi kinachowakilisha njeo inayoonesha hali ya kuendelea kwa tendo ni “ka” na “na” katika uyakinishi na katika ukanushi ni kiambishi ***{z+----Ti}*** hutumika**.** Jediwali lifuatalo lina thibitisha ukweli wa madai hayo.

**Jedwali na 4.13: Kiambishi Hali "ka" kinachowakilisha Kuendelea kwa Tendo**

| Kitenzi | Nafsi | Lahaja ya kitumbatu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|---|
| Cheza<br>Piga | N1 umoja | nivu n***ka***soma | Nivu***si***somo | nilikuwa nikisoma | nilikuwa sisomi |
| | N1 wingi | twevu tu***ka***soma | twevu ***ha***tusomo | tulikuwa tukisoma | Tulikuwa hatusomi |
| | N2 umoja | kuvu u**ka**piga | kuvu *hu*pigi | ulikuwa ukipiga | Ulikuwa ukipiga |
| | N2 wingi | mevu m***ka***piga | muvu ***ha***mpigi | Mulikuwa mukipiga | Mulikwa hamupigi |
| Pika | N3 umoja | Kevu a***ka***pika | Kevu ***ha***piki | Alikuwa akicheka | alikuwa hacheki |
| | N3 wingi | wevu wa***ka***pika | Kevu ***ha***wapiki | Walikuwa wakipika | Walikuwa hawapiki |

**Chanzo: Data kutokaUwandani (2017)**

## 4.3 Uchambuzi wa Kimofosinaksia

### 4.3.1 Athari za Kimofofonolijia zinazojitokeza katika Lahaja ya Kitumbatu

Katika sehemu hii mtafiti ataangazia uchambuzi wa kimofofonolojia ulivyoathiri vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu. Lahaja ya Kitumbatu ina viambishi njeo vinavyowakilisha nyakati mbali mbali ambavyo huathiriana na viambishi vya nafsi kupelekea miundo ndani kwenda muundo nje na kujenga mjengeko mwingine wa vitenzi.

### 4.3.2 Athari za Kimofofonolojia zinazojitokeza katika Lahaja ya Kitumbatu Katika Njeo ya Wakati uliopita kwa Kitenzi cha Kawaida Uyakinishi

Data iliyowasilishwa kwenye jedwali na: 4.1 inaonesha kuwa kiambishi njeo kinachowakilisha wakati uliopita kwenye hali ya uyakinishi katika lahaja ya Kitumbatu ni tangamano la irabu **(z+----Ti).** Athari ya kimofafonolojia inayojitokeza katika hali hii ni utangamano uliopo kati ya irabu ya mzizi wa kitenzi na irabu ya utamatishi wa kitenzi chenyewe. Irabu ya mzizi wa kitenzi hufanana moja kwa moja na irabu tamatishi ya kitenzi hicho kama inavyoonekana hapo chini kwenye jedwali Na: 4.14

**Jedwali na.4.14 Vitenzi vya Kitumbatu Vinavyoonesha Wakati Uliopita Yakinishi katika Nafsi ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu**

| **Nafsi** | **Lahaja ya Kitumbatu** | | | **Maelezo ya kiswahili sanifu** |
|---|---|---|---|---|
| | **Kitenzi** | **irabu ya mzizi** | **irabu ya mwisho** | |
| N1-umoja | Nifanya<br>Nipaka | -a-<br>-a- | -a-<br>-a- | lifanya<br>nilipaka |
| N1-wingi | Tucheke<br>Tulisema | -e-<br>-e- | -e-<br>-e- | tulicheka<br>tulisema |
| N2-umoja | Kupiki<br>Kutii | -i-<br>-i- | -i-<br>-i- | ulipika<br>ulitia |
| N2-wingi | Mogo<br>Moto | -o-<br>-o- | - o-<br>-o- | mulioga<br>muliota |
| N3-umoja | kanunu | -u- | -u- | alinuna |
| N3-wingi | Wanunu | -u- | -u- | wamenunua |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

Kanuni ya tangamano la irabu limejitokeza pale ambapo irabu ya mzizi hufanana na irabu ya mwisho ya kitenzi, kutokana na hali hii maumbo ya vitenzi vya Kitumbatu vinavyowakilisha wakati uliopita huwa kama ilivyoonekana hapo juu na athari ya kimofofonolojia inayojitokeza ni kule kufanana kwa irabu ya mzizi na irabu tamatishi ya kitenzi.

### 4.3.3 Athari za Kimofofonolojia Zinazojitokeza katika Hali ya Ukanushi

Katika hali ya ukanushi kiambishi ambacho kinawakilisha njeo ya wakati uliopita katika lahaja ya Kitumbatu ni {-***e***-}. Jedwali lifuatalo linathibitisha madai yaliyodhihirishwa na mtafiti hapo juu.

**Jedwali na 4.15Vitenzi vya Kitumbatu vinavyoonesha Wakati uliopita Kanushi**

| **Nafsi** | **Lahaja ya Kitumbatu** | | **Maelezo ya Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|---|
| N1-umoja | si-*e*-sema<br>si-e-piga | S*e*sema<br>S***e***piga | sikusema<br>sikupiga |
| N1-wingi | hatu-e-sema<br>hatu-*e*-piga | Hat***we***sema<br>Hat***we***piga | hatukusema<br>hatukupiga |
| N2-umoja | hu-*e*-sema<br>hamu-e-soma | H***we***sema<br>Ham***we***soma | hukusema<br>hamukusoma |
| N3-umoja | ha-e-pika<br>ha-e-gonga | Hepika<br>H***e***gonga | hakupika<br>hakugonga |
| N3-wingi | hawa-e-pika<br>hawa-e-pangusa | Haw***e***pika<br>Haw***e***pangusa | hawakupika<br>hawakufuta |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

Jedwali liliopo hapo juu, linaonesha maumbo kadhaa ambayo yanadhihirisha miundo ya ndani ya vitenzi vya Kitumbatu vinavowakilisha wakati uliuopita katika hali ya ukanushi kwenye nafsi zote tatu katika hali ya umoja na wingi, maumbo hayo yanaonesha kuwa lahaja ya Kitumbatu inatumia mofu {***-e-***} kuwakilisha mofimu ya njeo inayowakilisha wakati uliopita katika hali ya ukanushi. Kwa hivyo vitenzi vya Kitumbatu vinavyowakilisha njeo ya wakati uliopita vinatofautiana kutoka miundo ndani kuelekea miundo nje inayosababishwa na njeo ya wakati inayotumika katika hali hiyo. Hali hii inajitokeza dhahiri katika nafsi ya kwanza umoja na nafsi ya tatu umoja na wingi. Hii ni athari ya kimofofonolojia iliyotawaliwa na kanuni ya udondoshaji ambayo imetumika katika nafsi mbili hizi. Kanuni hii inaonesha kwamba irabu /a/ hudondoka katika mazingira ya kuathiriana na irabu /e/ inayowakilisha njeo ya wakati uliopita. Baada ya kudondoka irabu /a/ na inayobakia ni irabu /e/ kamama inavoonekana hapo juu.

Katika nafsi ya kwanza wingi na nafsi ya pili umoja na wingi kanuni ya uyeyushaji imetumika. Kanuni ya uyeyushaji imetokea pale ambapo irabu /u/ katika mazingira ya kuathiriana na irabu /e/ inayowakilisha njeo ya wakati uliopita. Katika mazingira hayo irabu /u/ huyeyuka na kuwa kiyeyusho /w/. Hii ni athari ya wazi ya kimofofonolojia iliyosababishwa na kiambishi njeo cha wakati uliopita katika lahaja ya Kitumbatu.

Hivyo inaonekana kuwa kanuni zinazotawala mabadiliko ya kimofofonolojia kwenye ukanushi njeo ya wakati uliopita ukanushi katika lahaja ya Kitumbatu ni udondoshaji kwa upande mmoja na uyeyushaji kwa upande wa pili. Njeo ya wakati uliopita ukanushi ndiyo chachu iliyogeuza muundo ndani kwenda muundo nje

kupitia athari za kimofosintaksia. Kimofolojia kanuni hizi zinaweza kuwasilishwa ***/a/→[Φ] /-/ έ / kwenye udondoshaji na*** **/u/→[w]** /έ/ kwenye uyeyushaji.

## 4.4 Athari za Kimofofonolojia Zinazojitokeza Kwenye Vitenzi vya Lahaja ya Kitumbatu Katika Njeo ya Wakati Uliopita Katika Hali ya Uyakinishi na Hali ya Ukanushi

Data inaonesha kuwa katika vitenzi vya Kitumbatu njeo inayowakilisha wakati uliopo ni {-na-} katika hali ya uyakinishi na ukanushi, kwa hivyo katika vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu hakuna miathiriano yoyote ya kimofofonolojia inayojitokeza katika njeo inayowakilisha wakati uliopo katika hali ya uyakinishi na ukanushi. Jedwali lifuatalo linathibitisha.

**Jedwali na. 4.16 Vitenzi vya Kitumbatu Vinavoonesha Wakati Uliopo Katika Hali ya Uyakinishi na Ukanushi**

| **Kitenzi** | **Lahaja ya kitumbatu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| | Uyakinishi | Ukanushi | uyakinishi | ukanushi |
| Anguka | N***na***kugwa<br>tu***na***kugwa | si***na***kugwa<br>hatu***na***gwi | ninaanguka<br>tunaanguka | sianguki<br>hatuanguki |
| Cheka | Ku***na***cheka<br>mu***na***cheka | hu***na***cheka<br>hamu***na***cheka | unacheka<br>munacheka | hucheki<br>hamucheki |
| taka | Ka***na***taka<br>wa***na***taka | ha***na***taka<br>hawa***na***taka | anataka<br>wanataka | hataki<br>hawataki |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

Kiujumla data inaonesha kuwa katika kitenzi cha Kitumbatu kwenye njeo inayowakilisha wakati uliopo katika hali ya uyakinishi na ukanushi hakuna miathiriano ya kimofofonolojia kwa kuwa hakuna kipashio cha njeo wala nafsi ya umoja wala wingi iliyoonesha muathiriano.

## 4.5 Athari za Kimofofonolojia zinazojitokeza katika Wakati Ujao

Data inaonesha kuwa katika vitenzi vya Kitumbatu njeo inayowakilisha wakati ujao ni {-ta -} katika hali ya uyakinishi na ukanushi, kwahiyo katika vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu hakuna miathiriano yoyote ya kimofofonolojia inayojitokeza katika njeo inayowakilisha wakati ujao katika hali ya uyakinishi na ukanushi. Jedwali lifuatalo linathibitisha

**Jedwali na 4.17 Vitenzi vya Kitumbatu vinavyoonesha Njeo inayowakilisha Wakati Ujao**

| **Kitenzi** | **Uyakinishi** | **Ukanushi** | **Uyakinishi** | **Ukanushi** |
|---|---|---|---|---|
| Pika | N***ta***pika<br>tu***ta***pika | Si***ta***pika<br>hatu***ta***pika | nitapika<br>hatu***ta***pika | si***ta***pika<br>hatu***ta***pika |
| Sema | Ku***ta***sema<br>mu***ta***sema | Hu***ta***sema<br>hamu***ta***sema | Utasema<br>mutasema | hutasema<br>hamutasema |
| Lia | Ka***ta***lia<br>watalia | Ha***ta***ia<br>hawa***ta***lia | Atalia<br>Watalia | hatalia<br>hawatalia |

**Chanzo:Data kutokaUwandani (2017)**

Kiujumla data inaonesha kuwa hakuna miathiriano iliyojitokeza katika kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati ujao katika hali ya uyakinishi na ukanushi katika kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu.

## 4.6 Athari za kimofofonolojia zinazojitokeza katika Njeo inayowakilisha Hali Timilifu

Kama ilivyo kwa njeo inayowakilisha wakati uliopo na wakati ujao kwamba hakuna miathiriano ya kimofofonolojia na ndivyo ilivyo kwa njeo inayowakilisha hali timilifu data ifuatayo inathibitisha.

**Jedwali na. 4.18Vitenzi vya Kitumbatu vinavyowakilisha Hali Timilifu**

| **Kitenzi** | **Lahaja ya Kitumbatu** | | **Kiswahili Sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| Onja | ni***ma***onja<br>tu***ma***onja | Si***ja***onja<br>ha***tu***jaonja | nimeonja<br>tumeonja | sijaonja<br>hatujaonja |
| Poa | ku***ma***poa<br>mu***ma***poa | Hu***ja***poa<br>hamu***tu***japoa | umepoa<br>tumepoa | hujapoa<br>hamujapoa |
| nyamaza | ka***ma***nyamaza<br>wa***ma***nyamaza | ha***ja***nyamaza<br>hawa***ja***nyamaza | amenyamaza<br>wamenyamaza | hajanyamaza<br>hawajanyamaza |

**Chanzo:Data kutoka uwandani (2017)**

## 4.7 Athari za Kimofofonolojia zinazojitokeza katika Hali ya Mazoea

Katika hali ya mazoea vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu havikupata athari yeyote ya mofofonolojia, wala hakuna kiambishi kinachoonesha tofauti ya nafsi ikiwa ya kwanza, ya pili au ya tatu, isipokuwa katika hali ya ukanushi sentensi zifuatazo zinaonesha hali hiyo katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali na: 4.19 Vitenzi vya Kitumbatu vinavyoonesha Njeo inayowakilisha hali ya mazoea**

| Kitenzi | Lahaja ya Kitumbatu | | Kiswahili Sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| | Uyakinishi | Ukanushi | uyakinishi | ukanushi |
| Cheza | mie hucheza usiku . sue hucheza usiku. | mie sicheze usiku sue hatucheze usiku | mimi hucheza usiku sisi hucheza usiku | mimi sichezi usiku sisi hatuchezi usiku |
| Osha | weye huosha unju nyie huosha unju | weye huoshounju nyie hamuoshounju | wewe huosha asubuhi nyinyi hamuoshi asubuhi | wewe huoshi asubuhi nyinyi hamuoshi asubuhi |
| Poka | yeye hupoka wana wao hupoka wana | yeye hapoko watoto wao hawapokowana | yeye hupokonya watoto wao hupokonya watoto | yeye hapokonyi watoto wao hawapokonyi watoto |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)**

## 4.8 Ufaafu wa Kinadharia

Kama ilivyodokezwa na mtafiti kwenye sura ya pili nadharia iliyokusudiwa kutumika ni ile ya Mofofonolojia. Nadharia hii imeteuliwa kwa kuwa inaakisi moja kwa moja uchambuzi wa kazi hii uliofanyika. Nadharia hii kwa mujibu wa maelezo yaliyoko **(2.12)** inajihusisha na mambo matatu makubwa na ya msingi. Mambo hayo ni pamoja na kuchunguza viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu na

kubaini mabadiliko ya kimofofonolojia yanavyoathiri kiambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu ambayo ndiyo dhima ya nadharia hii. Katika kazi hii viambishi vinavyowakililisha njeo vimewekwa bayana kwenye majedwali yote yaliyowasilisha vitenzi. Hili limeenda sambamba na kuakisi kazi ya kwanza ya nadharia hii. Mabadiliko ya kimofofonolojia yaliyoibadilisha miundo ndani kuwa miundo nje ni mfano dhahiri uliyoiwezesha kanuni ya Mofofonolojia kudhihirisha ufaafu wake kwenye uchambuzi huu. Kanuni za uyeyushaji, udondoshaji na tangamano la irabu ni za Kimofofonolojia. Kudhihiri kwa mofu za njeo na hali, kujibainisha kwa mabadiliko kutoka muundo ndani kuja muundo nje, na kudhihiri mabadilko haya kupitia kanuni mbalimbali za kimofofonolojia ni ushahidi tosha wa kuonesha kufaa kwa kanuni teule.

## 4.9 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua malengo mawili ya utafiti. Lengo la kwanza limebainisha njeo za nyakati na hali mbalimbali zilizojitokeza. Lengo la pili limefafanua michakato ya kimofofonolojia kwa kubainisha mabadiliko ya miundo, kutoka muundo ndani kwenda miundo nje. Mabadiliko hayo yamedhihiri kupitia kanuni mbalimbali za kimofofonolojia. Kanuni hizo ni udondoshaji, uyeyushaji na tangamano lairabu.

# SURA YA TANO

## 5.1 Utangulizi

Utafiti huu ulihusika na"Kuchunguza Viambishi Njeo na Hali katika Lahaja ya Kitumbatu." Ambapo ulielezea malengo mawili ikiwa moja ni kubainisha viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu na la pili ni kuchanganua athari za kimofofonolojia zinazojitokeza katika vitenzi vya Kitumbatu wakati wa kudhihirisha viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika kisiwa cha Pemba, mkoa wa kusini, wilya ya Mkoani katika jimbo la Kiwani shehiya ya Mwambe na shehiya ya Jombwe. Katika shehiya ya Mwambe vijiji vilivyofanyiwa utafiti huu ni skuli ya Mwambe, Bwegeza, Kwasanani, Mchakwe na Chanjaani. Katika shehiya ya Jombwe ni kijiji cha Mkanjuni na Tomondo. Jumla ya watafitiwa 50 walishiriki wakiwemo waalimu, wanafununzi na wazee wenye umri kati ya miaka 53−70. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya dodoso, uchunguzi makini na usaili. Datazilichambuliwa kwa kutumia njia ya maelezo na pale ilipohitajika kutumia majedwali ilifanya hivyo.

Nadharia iliotumika katika utafiti huu ni nadharia ya mofofonolojia ambayo baadhi ya wanaisimu wameitumia katika katika tafiti zao.

## 5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Kitika lengo la kwanza la utafiti lililokusudia kubainisha viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu.Utafiti umebaini kwamba kuna tofauti kiasi katika viambishi vainavyowakilisha njeo mbali mbali za nyakati katika lahaja ya Kitumbatu

i) njeo ya waklati uliopita katika lahaja ya kitumbatu huwa *(z+-----$T_i$)* katika uyakinishi na katika ukanushi huwa {-e-), ii) njeo ya wakati uliopo katika lahaja ya Kitumbatu katika hali ya uyakinishi na ukanushi huwa (-na-). iii) Katika wati ujao vitenzi vya Kitumbatu huambikwa kiambishi (-ta-) katika hali ya uyakinishi na katika hali ya ukanushi. iv) Katika hali timilifu vitenzi vya kitumbatu hubeba kiambishi (-ma-) katika hali ya uyakinishi na katika hali ya ukanushi hubeba kiambishi (-ja-). v) Katika hali ya kuendelea kwa tendo huambikwa kiambishi (-ka-) au kiambishi (-na-). vi) Katika hali ya ushuruti huambikwa viambishi vya aina mbili ambapo kiambisi kimoja huwa (-ngali-) au (-nge-) katika uyakinishi na katika ukanushi hubeba (-si-) na kingine ni kiambishi (-ki-) katika uyakinishi na katika ukanushi hubeba kiambishi (-si-) pamoja na mofimu ya urejeshi (-po-).

Na katika lengo la pili ambalo linalenga kuchanganua athari za kimofofonolojia zinazojitokeza katika vitenzi vya Kitumbatu wakati wa kudhihirisha viambishi njeo na hali. Katika lengo hili imedhihirika kuwa vitenzi vya Kitumbatu huruhusu miathiriano ya kimofofonolojia inayopelekea mabadiliko ya miundo ya vitenzi vya Kitumbatu, miathairiano hii hutokea kwa baadhi ya nyakati, kama vile: a) wakati uliopita yakinishi utafiti unaonesha kuwa hutokea tangamano la irabu na katika hali ya ukanushi. Mabadiliko hayo hujitokeza huku yakiathiriwa moja kwa moja na kanuni za mofofonolojia. Kanuni zilizotawala zaidi mabadilko hayo ya kimofofonolojia ni udondoshaji na uyeyushaji. Mabadilko hayo yamedhihirisha wazi wazi maumbo ya vitenzi vya Kitumbatu.

## 5.4 Hitimisho

Mtafiti amebaini kuwepo viambishi njeo vya Kitumbatu vinavyotofautiana na vile vya Kiswahili Sanifu, ila havina uwezo wa kuwatenga Watumbatu kiasi cha kutokuelewana na waongeaji wa lahaja Sanifu.

## 5.5 Mapendekezo

Mtafiti wa kazi hii anapendekeza kwamba, tafiti nyingine zinazohusu uchambuzi wa kimofofonolojia za lahaja zifanyike, ili kubaini jinsi viambishi vya njeo vinavyoathiri vitenzi vya lahaja husika. Pili, mtafiti amependekeza kwamba tafiti nyingine za Kimofofonolojia zifanywe kwenye lugha za Kibantu ili kubaini kwa kiasi gani vitenzi vya Kibantu huathirika kutokana na michakato ya kimofofonolojia.

## MAREJELEO

Abdulla, A. S. (2016). "Viambishi Njeo Katika Lahaja ya Kipemba." Tasinifu ya ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kukuu Huria Tanzania

Adam, J. and Kamuzora, F. (2008). *Research Methody for Graduate Bussinessans and Socialstudies. Morogoro:* Mzumbe Book Project.

Ali, M. M. (2016). "Athari za Utandawazi katika Lahaja ya Kitumbatu." Tasinifu ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Bakar, K.B (2015). "Ulinganishi wa Kiisimu Kati ya Lahaja ya Kipemba na Kitumbatu." Tasnifu ya Uazamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

BAKIZA (2010). Kamusi ya Kiswahili Fasaha. Zanzibar: Baraza la Kiswahili la Zanzibar.

Chomsky, N. (1957). *Some General Propaties of Phonological Rules*.

Cohen, L. M. & Morrison, K. (2000). *Research Methods in Education.* Toleo la 5. London Rutlegefalme.

Enon, J. (1995). *Education Research Statisticand Field study.* Kampala Makerere University of Uganda

Enon, J. (1998). *Research Methods in Special Education and Feild Study*. London: Oxford.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi. JKF.

Hamad, S. O. (2011) *Tense Aspect Dissertation.* University of Dar es Salaam.

Helen, C. B. (2013). "Muundo wa Kimofosintaksia wa Kitenzi (Kt), cha Kinandi." University of Estern -Africa-Baraton-Kenya.TUKI (1990). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y. M. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili* (SAMAKISA) Dar eS Salaamu: TUKI.

Kombo, D. K. and Trampo, D. I. (*2006). Proposal Thises Writing an Introduction.*Nairobi.

Kothari, C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques. New Delhi:*New International Publishing Ltd.

Maganga, C. I. (1991). "A Study of Mofofonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi." M.A Diseration of the University of Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. & Msanjila, Y. P (1997) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu Sekondari na Vyuo* (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.

Mathoko, P. M. (2007). *Isimu Jamii Misingi na Nadharia.* Nairobi: Nairobi University Press.

Mazurui, A. M. (1993). *Aspect Marking Swahili: According to Variation.* TUKI: Dar es Salaam.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu, Fonetiki na Fonolojia, Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: JKF.

Suluhaya, M. C. (2010) *Kiswahili 1. Nadharia ya Lugha Kidato cha Tano na Stia*. Dar es Salaam-childreneducation (cheso).

Waziri, M. M. (2016). "Kuchunguza Nyimbo za Singo katika Kijiji cha Uzini Zanzibar." Tasinifu ya Uzamili ya Kiswahili ya ChuoKikuu Huria Cha Tanzania

Whitely, W. H (199). *Swahili, The Rise of National Language*. London: Methuen.

William, N. (2011). *Your Research Project – A Step-By- Step Guile for the First Time*, SAGE Publications: London.

## VIAMBATISHO

Kiambatisho Na :1

Jinakamaukipenda -----------------------------------------

Umri------------------------------------

Mahalaunapoishi----------------------

Mtaa au kijiji-------------------------------

Kazi ------------------------

Jinsi-------------------------

Umri-------------------

**1)** Andika v––itenzizivifuatavyo vya Kiswahili Sanifu kama vinavyo tamkwa katika lahaja ya kitumbatu

Kiswahili Sanifu Kitumbatu

Uyakinishi____________________________________________ukanushi

Ninacheza____________________________________________sichezi

Unacheza____________________________________________huchezi

Munacheza____________________________________________hamuchezi

Anacheza____________________________________________hachezi

Wanacheza____________________________________________hawachezi

Niliiimba_______________________________________________sikuimba

tuliimba________________________________________________hatukuimba

Uliimba________________________________________________hukuimba

Muliiimba______________________________________________hamukuimba

Aliimba________________________________________________hakuimba

Waliimba______________________________________________hawakuimba

Nitasoma_______________________________________________sitasoma

Tutasoma_______________________________________________hatutasoma

Utasoma________________________________________________hutasoma

Mutasoma______________________________________________hamutasoma

Atasoma________________________________________________hatasoma

Nimesoma______________________________________________sijasoma

Tumesoma______________________________________________hatujasoma

Mumesoma_____________________________________________hamujasoma

Amesoma______________________________________________hajasoma

Wamesoma_____________________________________________hawajasoma

Husoma________________________________________________hasomi

Ningecheza____________________________________________nisingecheza

Akicheza______________________________________________asipohachezi

a) Katika Kiswahili sanifu kiambishi “KI”na,”NA".hutumika katika hali ya ushuruti na katika hali ya kuendelea kwa tendo, , unaweza kuonesha lahaja ya Kitumbatu hutumia viambishi gani katika hali hizo.

Kiswahili sanifu_________________Kitumbatu

Alikuwa akisoma ________________kevu akasoma

Akicheza hasemi_________________akacheza hasemi

Alikuwa anasoma._______________ Kevu akasoma.

**Kiambatisho Na:2**

Muongozo Wa Maswali Ya Hojaji Kwa Wazee Wa Vijiji Vya Shehia Ya Mwambe Na Jombwe Katika Wilaya Ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba Zilizotumika Kutumika Katika Utafiti Huu.

MADA: Uchunguzi Wa Viambishi Njeo Na Hali Katika Lahaja Ya Kitumbatu.

Jina La Mtafiti-----------------------------------------------Tarehe-----------------------------

Mimi ni mtafiti ambaye ninafanya utafiti unaohusu uchunguzi wa viambishi njeo na hali katika lahaja ya Kitumbatu, hivyo naomba ushirikiano wako katika hali zote

tunaomba utueleze jina lako,

umri ,

mtaa\kijiji unachoishi

viambishi njeo na hali nai viambishiambavyo huonesha nyakati mbali mbali na hutokea baada ya kiambishi cha nafsi kwa mfano:-

a-**na**-som-a

kiambishi ambacho kimekozeshewa wino ni kiambishi cha wakati uliopo.

Tunaomba ushirikiane na sisi ili uweze kutupatia vitenzi vitatu vitatu vya kitumbatu vinavyoonesha nyakati mbali mbali katika lahaja hiyo.

1.Wakati Uliopo

Ninasoma

Sisomi

Ninaimba

Siimbi

Unaimba

Huuimbi

Anacheza

Hachezi

2.Wakati ujao

Atataka

Hatataka

Utalima

Hutalima

3.Wakati uliopita

Nilicheza

Sikucheza

Ulicheza

Hukucheza

Alicheza

Hakucheza

4, Hali ya Mazoeya

Hucheza

Sichezi

Hucheza

Hachezi

Hucheza

Huchezi

5.Hali ya kuendelea kwa tendo

Alikuwa anapika

Alikuwa apiki

Alikuwa anataka kupika

Alikuwa hataki kupika

Nilikuwa ninapika

Nlikuwa sipiki

6. Hali timilifu

Ameimba

Hajaimba

America

Hajafika

Amependa

Hajapenda

7. Hali ya kudadisi kwa tendo\ushuruti

Engekuja

Angelikuja

Akisoma